# Nipashe

Jumatano Februari 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580844

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 896,686,220

NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#




**Soko** lingine lateketea kwa moto

UKURASA 3



MBAPPE, MADRID WAFIKIA MAKUBALIANO

UKURASA 22

# Tulia: Bunge litaihoji serikali kwa hekima

UKURASA 2



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akipongezwa na maspika wastaafu Anne Makinda (kushoto) na Pius Msekwa, baada ya kuchaguliwa bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**MRITHI WA MAALIM SEIF ACT AANZA NA UCHUMI**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, amesema hataweza kuufikia uongozi...

UKURASA WA 8

**BOMBA MAFUTA KUVUTIA UWEKEZAJI WA TRILIONI**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema makadirio ya dola bilioni 3.5 (Sh. trilioni 8,042) yanatarajiwa...

UKURASA WA 19

**DARAJA TANZANITE LILIVYOWAKUNA DAR**

DARAJA la Tanzanite lililojengwa juu ya bahari kutoka eneo la Aga Khan mpaka Oysterbay lilianza kutumika jana, huku...


## Ahueni kwa watumiaji bei za mafuta kushuka

UKURASA 3



Lissu



Saanane

## Lissu, Lema, Ben Saanane watajwa kesi ya Mbowe

UKURASA 2


MICHEZO **NABI AWASHUKIA WACHEZAJI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Magari yakipita katika Daraja la Tanzanite, baada ya kukamilika na kufunguliwa rasmi kwa matumizi, jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk 19. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tulia: Bunge litaihoji serikali kwa hekima

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

BUNGE limemchagua kwa kura zote 376, Dk. Tulia Ackson kuwa Spika, mara baada ya kunadi hoja zake na wenzake wanane wa vyama vya upinzani.

Baada ya kula kiapo cha kushika madaraka hayo makubwa kwenye chombo hicho cha kutunga sheria, Dk. Tulia aliahidi kuwa Bunge chini ya uongozi wake, litaihoji serikali kwa hekima na busara ili wananchi wapate maendeleo.

Jana shughuli ya Bunge ilikuwa ni kumpata Spika, uchaguzi uliooongozwa na mbunge mkongwe kuliko wote, Willium Lukuvi, aliyemtangaza Dk. Tulia kuwa mshindi.

Baada ya kutangazwa, Dk. Tulia alipelekwa mbele kwa shangwe na alipoapa, alisindikizwa hadi nje ya Bunge na Mwenyekiti huyo na baadaye kuingia ndani ya Bunge hilo akiwa kwenye mavazi rasmi ya Spika, akimwapisha mbunge mpya wa Jimbo la Ngorongoro, Emmanuel Shangai.

"Heshima mliyonipa, mmenipa kura zote za wabunge wote waliohudhuria siku ya leo, nawashukuru sana. Tulikuwa wagombea 71 tuliopata haki sawa, ukomavu wa kidemokrasia ndani ya CCM ni wa kupigiwa mfano," alisema.

Aliwashukuru wabunge hao kwa imani waliyomwonyesha ambayo itakuwa chachu ya utendaji katika kuliongoza Bunge.

Alimshukuru aliyekuwa Spika, Job Ndugai, kwa kumpa fursa na kumfundisha mambo mbalimbali ambayo yalimsaidia kufanya kazi yake kwa ufanisi.

HEKIMA NA BUSARA

Dk. Tulia alisema dira za kuongoza kazi ya Bunge ni hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Aprili 22, mwaka 2021, ambaye aliainisha vipaumbele vya serikali ya awamu ya sita ikiwamo kuimarisha uchumi wa nchi, nidhamu, kusimamia rasilimali za nchi, kuboresha huduma za kijamii, uwajibikaji na kuwajibisha wazembe.

Alisema wabunge kazi yao imeainishwa kwenye Katiba ibara ya 63 kwamba ni ndicho chombo kikuu chenye madaraka na wajibu kwa niaba ya wananchi kusimamia na kuishauri serikali katika majukumu yake.

Dk. Tulia alisema Bunge ni daraja na atatumia nguvu zake kuliongoza kwa umakini ili liwe daraja madhubuti kati ya wananchi na serikali na ataliongoza kuishauri serikali ili kutimiza wajibu wake.

"Tutauliza maswali, kuhoji serikali kwa hekima na busara, tutafanya kwa nia thabiti ili wananchi wapate maendeleo wanayotamani na kupiga hatua katika nyanja zote za maendeleo," alisema.

ILIVYOKUWA ASUBUHI

Baada ya wabunge kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge, Mwenyekiti wa Bunge, Mussa Zungu, alimkaribisha Katibu wa Bunge ambaye alisoma barua ya Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyetangaza kujiuzulu nafasi hiyo baada ya kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kugombea nafasi ya Spika.

Baada ya kusomwa kwa barua hiyo, Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, alimtangaza Mbunge wa Jimbo la Isimani, Lukuvi, kwa nafasi yake ni mbunge wa muda mrefu ambaye ameishika tangu mwaka 1995.

Baada ya tangazo hilo, Mwenyekiti wa muda, Zungu alitangaza kuahirisha kwa muda shughuli za awali za Bunge na Lukuvi kukaribishwa kukalia kiti hicho kwa ajili ya uchaguzi wa Spika, akiwaita wagombea mmoja baada ya mwingine kujieleza na kuomba kura.

Kwa mujibu wa kitabu cha orodha ya wabunge, Bunge hilo linaundwa na jumla ya wabunge 354 wa CCM, 20 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha Wananchi CUF watatu, ACT-Wazalendo wanne na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Uchaguzi huo umefanyika kutokana na kujiuzulu kwa Ndugai katika nafasi hiyo ya uspika.

## KESI YA MBOWE

# Lissu, Lema, Ben Saanane watajwa

**Na Kulwa Mzee**

LUTENI Dennis Urio amedai hafahamu kama aliyekuwa mgombea urais, Tundu Lissu na Godbless Lema wako uhamishoni kwa sababu walinyang'anywa walinzi ambao ni mshtakiwa wa kwanza, pili na watatu wanaotuhumiwa kwa ugaidi.

Shahidi huyo wa 12 amedai hafahamu kuwa aliyekuwa msaidizi wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, Ben Saanane kapotea mpaka leo hajulikani aliko na hafahamu kama msanii Diamond au wacheza mpira wana walinzi.

Hayo yalidaiwa jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mbele ya Jaji Joackim Tiganga wakati shahidi akihojiwa maswali na Wakili Peter Kibatala katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mbowe na wenzake watatu.

Akitoa ushahidi alidai hajawahi kuwekwa kizuizini na anashangaa kumsikia wakili akimwambia yuko chini ya ulinzi, hayuko huru na anapokuja mahakamani anasindikizwa na maofisa wa jeshi wenye silaha.

Shahidi alidai hamfahamu John Urio anayedaiwa kuwa baba yake mdogo na hoja kwamba gari lake aina ya RAV4 lilikuwa limeshikiliwa, aliyelitoa ni mkewe na alilifuatilia kwa viongozi wa jeshi kwa muda mrefu.

Wakili Kibatala alimwambia shahidi kuwa mwanaye Jackson alipozaliwa Desemba 17, mwaka 2020, alikuwa kizuizini akapelekewa mtoto huko alipokuwa mafichoni.

"Yaani mtoto azaliwe halafu niletewe kizuizini, jaribu kufikiria kidogo wakili msomi, sijawahi kuwekwa kizuizini," alidai shahidi.

Alidai katika ushahidi wake hajazungumzia kitu kuhusu 'spray' ya sumu au poda ya sumu.

Luteni Urio alidai hafahamu mshtakiwa Halfani Bwire na wenzake walihusika kumlinda Lissu wakati anawasili Tanzania kwa ajili ya uchaguzi mwaka 2020.

Shahidi alidai Rais halindwi na makomandoo na hafahamu kama shughuli mojawapo ya vijana aliowatafuta ni kumlinda Lissu.

Luteni Urio alidai anafahamu Jeshi la Polisi kazi yake ni kulinda raia lakini Lissu alipigwa risasi na hafahamu kama mpaka leo Jeshi la Polisi hawajamkamata mtu hata mmoja aliyehusika kumpiga risasi Lissu. Alidai hafahamu kama Mbowe alikuwa na mlinzi anayeitwa Allah Bhujo, na hafahamu kuwa msaidizi wa Mbowe, Ben Saanane kapotea na hajulikani aliko.

Alidai Jeshi likifahamu amewasiliana na Mbowe siyo kosa ofisa wa jeshi kuwa na uhusiano binafsi na kiongozi wa kisiasa.

Luteni Urio alidai haikuwa bahati mbaya kumtafutia Mbowe walinzi ndiyo maana hakukamatwa kutokana na suala hilo.

Alidai anafahamu kuwa CHADEMA ilikuwa na mgombea urais lakini hafahamu kama alizunguka nchi nzima kufanya kampeni na hakufahamu kuwa moja ya kazi ya washtakiwa ni kulinda makao makuu ya CHADEMA.

Shahidi alidai hafahamu kama fedha alizopewa kusafirisha vijana zilikuwa za Mbowe au zilitolewa na CHADEMA kwa kufuata utaratibu.

Alidai hafahamu kama Diamond au wachezaji mpira wana walinzi.

Akiendelea na ushahidi, alidai anajua tukio la kula njama kufanya ugaidi lilitokea kati ya Julai Mosi na 10, yaliyoandikwa katika hati ya mashtaka kwamba tukio lilitokea Mei Mosi hakusema yeye.

Shahidi akijibu maswali ya Kibatala, alidai hana taarifa kama Godbless Lema yuko uhamishoni, hafahamu kama Lissu yuko uhamishoni au kaenda kutalii.

Alidai hafahamu kama washtakiwa, Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya wasingekamatwa Lissu angebaki nchini lakini kanyang'anywa walinzi wake.

Pia alidai hafahamu kuwa kijana mmoja kati ya hao watatu, alikuwa kapangwa kumlinda Lema.

Wakili Kibatala alimaliza kumhoji shahidi huyo wa Jamhuri kutokana na ushahidi wake na kuwaachia Jamhuri kumhoji kama wana maswali ya ziada.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Kasekwa, Ling'wenya na Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya ugaidi.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (kulia), akizungumza kwenye mkutano wa kujadili mradi wa majaribio wa kupinga unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kingono uliohusisha wajumbe wa Kamati ya Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto Mkoa wa Dar es Salaam (MTAKUWWA) na wadau wengine wanaojengewa uwezo wa kupambana na ukatili huo, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ahueni watumiaji kushuka bei za mafuta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza kupungua kwa bei ya petroli kwa Sh. 21 kwa lita huku dizeli ikiongezeka kwa Sh.13 katika Bandari ya Dar es Salaam.

Aidha, imeanzisha bei ya kikomo na bei ya chini ambazo zitaanza kutumika leo huku ikitahadharisha kuwapo na ongezeko la bei za mafuta kwa Machi na Aprili, mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema hatua hiyo inatokana na kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Alisema bei za rejareja za mafuta ya petroli na dizeli kwa mikoa ya kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimepungua kwa Sh. 123 lita (petroli) na Sh. 92 (dizeli).

"Bei za rejareja za mafuta ya petroli na dizeli kwa mikoa ya kusini ambayo ni Mtwara, Lindi na Ruvuma zinaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la Januari 5, mwaka huu. Hii ni kwa sababu kwa mwezi Januari hakuna shehena ya mafuta iliyopokewa kupitia Bandari ya Mtwara," alisema.

Kuhusu bei ya kikomo na ya chini, Mhandisi Chibulunje alisema katika kuhakikisha kunakuwa na ushindani sawa, bei hizo zitaanza kutumika leo, hivyo ununuaji wa mafuta kutoka kwenye maghala sasa ni bei mbili na muuzaji hatakiwa kuzidisha.

"Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei ya kikomo au kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa kama ilivyokokotolewa kwa kutumia fomula na kanuni za kupanga bei za mafuta za mwaka 2022," alisema.

Alibainisha kuwa katika bei ya kikomo ya mafuta ya petroli Sh. 2,350.54 (petroli), Sh. 2,208.51 (dizeli) na Sh. 2.161.76 (mafuta ya taa) kwa Bandari ya Dar es Salaam huku bei za chini zitakuwa Sh. 2,227.54 (petroli), Sh. 2,085.51 (dizeli) na Sh. 2,038.76 (mafuta ya taa).

Hata hivyo, alisema katika kufuatilia mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia, kuna uwezekano mkubwa wa kuongezeka kwa bei ya mafuta kwa Machi na Aprili, mwaka huu.

"EWURA itaendelea kufuatilia mwenendo huo kwa karibu ili kuishauri serikali hatua za kuchukua katika harakati za kupunguza makali ya bei ya mafuta," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, dereva wa bodaboda, Ally Hamisi, alisema pamoja na kutangazwa kushuka kwa bei za mafuta bado hazileti nafuu kwa mwananchi wa kawaida.

Naye dereva wa daladala, Damas Ezekiel, alisema kuwekwa kwa utaratibu wa bei ya kikomo na bei ya chini itachochea ushindani kwa wafanyabiashara wa mafuta na kuna uwezekano wakauziwa kwa bei nafuu.

# Soko lingine lateketea kwa moto, laacha hasara

**Na Anjela Mhando,** Moshi

Vibanda 350 vya wafanyabiashara wa bidhaa za chakula na matunda katika Soko la Mbuyuni Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro vimeteketea kwa moto usiku wa kuamkia jana na kuacha hasara kubwa.

Moto huo ni mwendelezo wa matukio ya kuungua kwa masoko katika maeneo mbalimbali nchini. Matukio ya karibuni ni la kuungua kwa Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam na la Mchikichini jijini humo, huku wafanyabiashara wakipata hasara kubwa.

Wafanyabiashara ambao bidhaa zao zimeteketea katika soko la Moshi, wamesema hali yao ni mbaya kutokana na kupoteza mali zao baada ya kushindwa kuziondoa ndani ya vibanda hivyo.

Walisema hasara waliyoipata ni kubwa na hawajui wafanye nini kwa sasa ili maisha yaende kwani wanategemea biashara hizo kujikimu kimaisha.

Rabia Safari, alisema wanaiomba serikali iwasaidie kwa kuwa wamechukua mikopo katika taasisi mbalimbali za fedha ili kuendesha biashara, hivyo hawaelewi watairudisha vipi.

Nae Ashura Ibrahimu aliiomba serikali iwaangalie wafanyabiashara wadogo kwani wanapata tabu, wengine ni yatima na wengine ni wajane ambao wamekuwa wakihangaika kujitafutia riziki na kwamba hawajui watapata wapi fedha kwa kuwa wamepoteza mitaji yote.

Akizungumza na wafanyabiashara wa soko hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, alisema kuwa moto huo ulianza usiku na hakuna mtu aliyedhurika.

Alisema vibanda takribani 350 viliteketeza, ingawa hakueleza thamani yake, huku akisema tathmini ya hasara inafanyika.

Kigaigai alitoa wiki tatu kwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kufanya ukarabati wa soko hilo ili kuwezesha wafanyabiashara hao kurejea katika maeneo yao.

Kagaigai alisema kuwa Serikali itahakikisha kila mfanyabiashara anarejea kwenye eneo lake na kuendelea na biashara. Pia alilitaka Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi katika eneo hilo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mkaguzu Abrahamu Ntezidyo, alisema kuwa chanzo cha moto huo hakijajulikana na kwamba ulisambaa katika eneo kubwa kutokana na upepo na msonganano wa vibanda vya mbao.




Hallmark Attorneys

EXIM BANK
Innovation is life

## NOTICE TO THE PUBLIC

## RECEIVERSHIP OF FIFTY (50) UNITS IN UHURU HEIGHTS TOWER– DAR ES SALAAM

We, Hallmark Attorneys and Exim Bank (Tanzania) Limited (the Bank), take note of various newspaper articles and press releases with misleading information, allegations and facts all issued and made on account of **COSMOS PROPERTIES LIMITED** (the Company) with regard to the ongoing Receivership and pending Court cases and would like to state the following:

1. That the Company is indebted to the Bank under various loan facility agreements and has defaulted the same.
2. That the Bank holds securities for the loans among others, legal mortgage over 50 units all in Uhuru Heights Tower registered in the Company's name.
3. That the Bank is lawfully entitled to proceed with recovery on account of the Company's default having issued all relevant statutory notices as required.
4. That the Receivership over the Company's properties as registered and advertised on 26th January 2022 is a valid and lawful process. Further that on 26th January 2022, the Company acting through its directors, employees and agents illegally and forcefully blocked and interfered with the Bank, Receiver and his agents from performing their lawful duties over the charged 50 units as required.
5. That there is pending High Court Civil Case no. 176 of 2021. However the suit relates to different claims as between the Company and the Bank. The matter being subjudice, we cannot comment on the substance or merits thereof and it is equally illegal for anyone else to do so.
6. That the alleged injunctive Court Order, if it exists, has not been procured or served on the Bank, the Receiver and or any of their agents as of the date hereof, as required or at all.
7. The Bank and the Receiver confirm that they have not attended any Court hearing where such order was sought or granted.
8. Further, if the said Court Order exists and subject to its receipt and review, neither the Bank and nor the Receiver will take any action contrary to the terms of a valid Court Order and shall be strictly and within the confines of the law, guided by what the Court has determined or will determine.

**IN VIEW OF THE FOREGOING**, the terms of the public notices issued on 26th January 2022 remain valid and subsisting and the public shall be kept informed on the developments.

**WALTER BUXTON CHIPETA**
**RECEIVER/MANAGER**
**C/O HALLMARK ATTORNEYS**
**18 RUVU/ CHOLE ROAD,**
**MASAKI AREA**
**P. O. BOX 13811,**
**DAR ES SALAAM.**
**Tel: +255 22 2601 314/6**
**Email: info@hallmarkattorneys.co.tz**

# Duni aanza na uchumi, siasa ACT

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, amesema hataweza kuufikia uongozi aliouonyesha Maalimu Seif Sharif Hamad kwa asilimia 100, lakini atatumia uzoefu wake kutimiza dhamira ya chama, ikiwamo matarajio ya kushika dola na kuwakomboa Watanzania kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Amesema kati ya maswali ambayo amekuwa akikumbana nayo kutoka kwa wanachama wake, waandishi wa habari pamoja na wananchi, ni iwapo atavimudu viatu vya Maalim Seif siku chache baada ya kuchukua nafasi ya uenyekiti taifa.

Duni aliyasema hayo jana kwenye mkutano na wahariri na waandishi wa habari uliofanyika mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi wakuu wa chama hicho, akiwamo Kiongozi wa Chama, Zitto Kabwe.

"Moja ya maswali ambayo ninyi waandishi, wanachama wa ACT-Wazalendo na wapenzi wa demokrasia nchini mmekuwa mkiniuliza, ni kama mimi nitaweza kuziba pengo la mtangulizi wangu, mkijiuliza kama nitaweza kuziba pengo la marehemu Maalim Seif.

"Ninaomba niseme bayana kuwa Maalim Seif hakuwa kiongozi wa kawaida. Viongozi wa aina yake hutokea mara chache duniani. Mimi sitaweza kulinganishwa na Maalim Seif. Lakini nawahakikishieni kuwa nami nina uzoefu wa muda mrefu wa kutosha wa muda mrefu na maarifa ya kutosha. "Nitayatumia katika kukiongoza chama kufikia mafanikio yake ya kushika dola na kuwakomboa Watanzania kiuchumi, kisiasa na kijamii," alisema.

Duni aliongeza kwamba maisha yake kisiasa, tangu enzi za chama kimoja hadi sasa, yamemwonyesha jinsi gani uvumilivu, unyenyekevu kwa malengo ya ukombozi wa watu, hulipwa kwa imani na mapenzi.

"Hata pale nilipopata misukosuko ya kesi nzito moja ya uhaini na nyingine ya kutuhumiwa kumuua askari huko Pemba, daima sikutetereka au kurudi nyuma. Ahadi yangu, nguvu na ari hiyohiyo nitakuwa nayo katika kuitumikia ACT-Wazalendo kwenye nafasi yangu ya Mwenyekiti wa Chama Taifa," alisema Duni.

Alisema kwamba kama mwenyekiti wa chama, ana wajibu wa kikatiba wa kuongoza vikao na kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao hivyo na masuala ya kipaumbele kwa kushirikiana na viongozi wenzake na wanachama.

Kadhalika, aliongeza kwamba atasimamia mageuzi ya uendeshaji wa chama kisasa ikiwamo kutekelezwa programu ya ACT Kiganjani, ili kuwezesha wanachama kusajiliwa na kulipia ada za uanachama kwa njia ya simu.

"Nitashughulikia masuala muhimu kitaifa. Mathalani bidhaa muhimu katika msimu huu wa kilimo, mbolea aina ya Urea imepanda kutoka Sh. 50,000 hadi 105,000 kwenye maeneo mengi.

"Hali ni hiyo hiyo kwenye bidhaa nyingi nchini, ikiwamo mahitaji muhimu kama vile vyakula, mafuta na vifaa vya ujenzi. ACT-Wazalendo itaendelea kupaza sauti juu ya masuala haya na mengine kuhakikisha kila Mtanzania anaishi kwa raha, furaha na ustawi," alisema Duni.

Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Othman Masoud Othman, alisema ndoto ya Maalim Seif, haimo tu kwenye kuchukua nafasi alizoshikilia, bali kwenye kuyatimiza yale aliyoyapigania.

"Sitayafanya hayo peke yangu. Maana kama ninavyosema kila siku, Maalim Seif alikuwa mkubwa kuliko sisi mmoja mmoja. Tunahitaji kuwa wengi na wamoja, ili kujaa kwenye nafasi ya Maalim Seif na kuyatimiza malengo yake. Mimi na wenzangu kwa umoja wetu na wingi wetu tutamhuisha Maalim Seif kwa kuitimiza ndoto yake kwa nchi hii na watu wake," alisema Othman.



Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Taifa, Juma Duni Haji, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza mikakati ya uongozi wake ya kukijenga chama hicho baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othuman Masoud Othuman. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwanafunzi auawa na kisha kunyofolewa sehemu za siri

**Na Waandishi Wetu**

WATU wasiojulikana wamemuua kikatili mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Tutuo, Sikonge mkoani Tabora, Maria Kazungu (13) na kisha kunyofoa viungo vyake vya siri wakati akienda kisimani kuchota maji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi (ACP) Richard Abwao, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kuahidi kukutana na waandishi wa habari ili kulizungumzia suala hilo.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Ngassa Kazungu, alisema jana kuwa Maria alitumwa Ijumaa na mama yake kwenda kuchota maji kisimani baada ya kutoka shuleni majira ya saa 11:00 jioni.

Kazungu aliweka wazi kuwa kwa mara ya kwanza mwanawe huyo alifuata maji na kurejea nyumbani salama lakini aliporudia kwa mara ya pili hakuonekana hadi siku ya pili mwili wake ulipookotwa kwenye kichaka ukiwa umenyofolewa viungo vyake katika sehemu ya siri huku masikio yakiwa yametobolewa na kitu chenye ncha kali.

"Nimepata pigo ambalo sitalisahau katika maisha yangu kwani mtoto wangu Maria ameuawa kikatili na mimi niliamua kumsomesha mwanangu ili siku za mbeleni aje kunisaidia lakini wameamua kukatisha maisha yake," alisema Kazungu huku akilia kwa uchungu.

Hata hivyo, Kazungu alisema anamwachia Mungu pamoja na Jeshi la Polisi kwa kuwa mauaji kama hayo hayapaswi kufumbiwa macho na vyombo vinavyohusika ni lazima vifanye kazi ili kuwabaini wanaofanya unyama kama huo.

Mwenyekiti wa Serikali Kitongoji cha Ulula, Masele Charles, alikiri kuuawa kwa mwanafunzi huyo na kwamba amesikitishwa na pia hajaridhishwa na mauaji hayo.

Mwenyekiti huyo aliweka bayana kuwa hivi sasa anategemea kuanza ulinzi mkali wa jeshi la sungusungu na polisi jamii katika kitongoji chake ili kukabiliana na vitendo vya uhalifu. Diwani wa Tutuo, Rashidi Magope, alionya kuwa waliofanya unyama huo pia walimtoboa mara tatu sikio la mkono wa kulia na kuongeza kwamba tukio hilo la kuuawa kwa mwanafunzi huyo ni la pili kwa kuwa hata mwaka jana aliuawa pia mwanafunzi wa shule ya sekondari.

Diwani huyo aliongeza kuwa mauaji hayo yanaleta taswira mbaya katika kata yake na kuwataka baadhi ya wananchi wanaojihusisha na vitendo kama hivyo kuacha mara moja. Aliliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kuwabaini wahalifu hao na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wilaya, John Palingo, alipoulizwa juu ya tukio hilo, licha ya kukiri kuwapo alisema yeye hakuwapo kwenye eneo la tukio kwa kuwa sasa yuko Dar es Salaam kwa matibabu.

**MAUAJI KIGOMA**

Jeshi la Polisi mkoa wa Kigoma limesema katika mwezi Januari, mwaka huu, kumetokea matukio saba ya mauaji yaliyosababisha vifo vya watu 10.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, alisema vyanzo vya mauaji hayo ni wivu wa mapenzi, ulevi na masuala ya kifamilia.

Katika moja ya matukio hayo, alisema kijana wa miaka 23, Herman John, mkazi wa kijiji cha Kinonko, wilayani Kakonko, Januari 5, mwaka huu, alimpiga mpini mama yake aitwaye, Celina Kasuga (63) ambaye alikuwa akimdai fedha yake Sh. 300,000.

Alisema katika tukio lingine, Januari 30 majira ya saa 4:00 usiku katika kijiji cha Nyarugusu wilaya ya Kasulu, watu watatu wanaotuhumiwa kuwa majambazi, waliuawa katika majibizano ya risasi na polisi.

Kamanda Manyama alisema katika tukio hilo, polisi walikamata silaha aina ya AK47 ikiwa na magazine mbili zenye risasi 47 na askari wao mmoja alijeruhiwa na yuko hospitalini akiendelea na matibabu.

"Miili ya majambazi hao iko hospitalini tunaomba ndugu wajitokeze kuchukua kwa sababu bado haijatambuliwa," alisema.

Pia alisema polisi wanamshikilia Mwenyekiti wa Kijiji cha Kabulanzwili, Joseph Bwebwe, na wenzake ambao walikutwa na silaha aina ya gobole zinazodaiwa kutumika kutekeleza uhalifu ikiwamo uwindaji haramu wa wanyamapori na ujambazi.

• **Imeandikwa na Jumbe Ismailly, Sikonge na Pendo Thomas, Kigoma.**

# Uteuzi Zuhura Ikulu waibua 'wakongwe'

**Na Romana Mallya**

WAKONGWE katika tasnia ya habari wamemmwagia sifa Zuhura Yunus Abdallah aliyeteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Mkurugenzi mpya wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, Rais amemteua Zuhura kushika nafasi hiyo kuanzia Januari 30 mwaka huu.

Kabla ya uteuzi huo, Zuhura alikuwa Mtayarishaji wa Vipindi na Mtangazaji wa Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) na amechukua nafasi ya Haniu ambaye atapangiwa kazi nyingine.

Wakizungumza na Nipashe kuhusiana na uteuzi huo, wakongwe wa tasnia ya habari walisema Zuhura anastahili nafasi hiyo kwa sababu ana uzoefu wa kitaifa na kimataifa.

Alakok Mayombo, mmoja wa wakongwe hao kwenye tasnia ya habari, alisema Zuhura siku zote amekuwa akifanya kazi yake kwa kufuata misingi ya taaluma.

"Ni mtu sahihi kufanya kazi Ikulu, ana uelewa mpana wa kitaifa na kimataifa. Kwa hiyo, atakuwa kwenye nafasi nzuri ya kufanya kazi na Rais," alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, alisema amefurahishwa na uteuzi huo kwa sababu uwezo wa Zuhura ni mkubwa na ni mtu mwenye ari, uelewa na taaluma, hivyo anaamini kila kitu kitakwenda vizuri.

"Zuhura ni mwandishi wa habari mzuri na vilevile ni mwandishi wa vitabu, ninachomfahamu ni kwamba upele umepata mkunaji," alisema.

Mwanahabari mkongwe, Absalom Kibanda, alisema Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ni ofisi binafsi ya Rais, hivyo Rais huteua mtu ambaye anamwamini, anamfahamu na mwenye uwezo.

"Zuhura amefanya kazi sehemu mbalimbali, nilikutana naye Radio Uhuru, akatoka akaenda magazeti ya Mwananchi kama mwandishi wa habari na mwanzoni mwa miaka ya 2000 kabla ya kwenda BBC ambako amefanya kazi kwa miaka 14, ana uzoefu wa kitaifa na kimataifa," alisema.

Zuhura ni mwanamke wa kwanza kutangaza kipindi cha Kiswahili cha Televisheni BBC, Dira ya Dunia akihudumu kwenye shirika hilo kwa miaka 14 na mwezi uliopita aliaga lakini hakusema alikokuwa anakwenda.

Alijiunga na shirika hilo mwaka 2008 akiwa mtangazaji na mtayarishaji wa matangazo na umaarufu wake ulipanda kila siku baada ya kuwa mtangazaji kinara wa matangazao ya redio, Dira ya Dunia.

Aliripoti Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa mwaka 2010 na katika kazi yake alihoji viongozi mbalimbali wa Afrika.

Miongoni mwao ni Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete kama sehemu ya taarifa kuhusu biashara haramu ya wanyamapori pamoja na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni.

Mwaka 2015 alifanya mahojiano na Edward Lowassa ambaye aligombea nafasi ya urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Amewahi kufanya kazi ya utangazaji katika vipindi mbalimbali vya redio ya Times FM na Uhuru FM.

TANGAZO

IITA Transforming African Agriculture 50 1967 - 2017

## POSITION ANNOUNCEMENT

### ZONE FACILITATOR

**IITA-TZ2022-R4D-002-NRS-TABORA**

**Background: The International Institute of Tropical Agriculture (IITA)** is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://www.iita.org/ for more information on IITA.

The project complements and builds on ongoing efforts from the Building an Economically Sustainable Seed System for Cassava in Tanzania (BEST Cassava) project that has operated since 2017 and will end this year and transition into the Building an Economically Sustainable, Integrated Cassava Seed System, Phase 2 (BASICS-II) project in 2022 in Tanzania

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the vacancy of the position of **Zone Facilitator** for the Muhogo Bora project.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in **Tabora, Tanzania.**

**Core Responsibilities**
The Zonal Facilitator will be responsible for CSE recruitment and selection of appropriate rural farmers with emphasis on women and youths, supervise training of CSEs, facilitate CSEs registration and ensure formation of CSE associations.

**The zonal project manager will be responsible for:**
- Ensuring Strategy and Performance
- Recruitment and selection of appropriate rural farmers with emphasis on women and youths to become CSEs
- A robust training program on agronomy, seed multiplication, and business skills
- Recruited CSEs to be registered as seed dealers by the Ministry of Agriculture (MoA)
- Linking CSEs with TOSCI for registration and inspections
- Backstopping, mentoring and monitoring for effective agronomic and business practices of CSEs
- Provide marketing and promotion support through seed grower's associations
- Build and strengthen the capacity of seed grower's associations
- Provide training to Extension staff (MoA) on commercialization and supervise them
- Management of other staff including performance– Field Area Facilitators (once recruited)
- Ensuring compliance with IITA procedures
- Administration and operation of Zonal Office
- Representing IITA in the local area business, government, other stakeholders
- Preparing monthly plans for the respective Zone and staff (to be approved by Technical Lead)
- Prepare monthly budget to correspond with activities in workplan
- Monitor expenses to budget - (staff expenses, vehicle, programming)
- Monitoring and Evaluation / Reporting
- Ensuring timely and accurate Data collection at all sites
- Monthly progress Zone report
- Tracking M&E against Performance targets and keeping Technical Lead advised
- Perform any other job-related duties as may be assigned by the supervisor.

**Qualification and Experience**
A Bachelors' degree in a relevant subject e.g. Agronomy, Agriculture general, Agribusiness
- A Minimum of 4 years' professional experience of working with Research, agri-business, marketing and farmer organizations in East Africa.
- Knowledge & practical experience of Cassava agronomy, Research, Plant protections, Value Chain Development
- Good command of spoken and written English
- Good communication/social skills; Good familiarity with the area the project/program is situated

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Tabora. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.
Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

IITA Transforming African Agriculture 50 1967 - 2017

## POSITION ANNOUNCEMENT

### FIELD PROJECTS MANAGER

**IITA-TZ2022-R4D-001-NRS- MOROGORO**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://www.iita.org/ for more information on IITA.

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) has won a competitive two-year grant from **IFAD- South-South Cooperation (SSTC)** Facility to implement a project on supporting the recovery of priority food crop value chains from the effects of COVID 19 to strengthen community resilience, markets, and trade development in Tanzania. The project will operate in the Central Corridor and part of the Lake Zone and will provide technical input and support to the IFAD-funded Agriculture and Fisheries Development Programme (AFDP). The two-year grant will be implemented in collaboration with the Alliance Bioversity International -CIAT (ABC) and other partners in target regions along the Central Corridor and part of the Lake Zone.

The second project is **BASICSII** which is a project funded by the Bill and Melinda Gates with a vision of developing and commercializing the cassava seed supply chain--from pre-basic seed of officially released varieties to the farmers through a network of government-certified commercial cassava seed entrepreneurs located throughout the primary cassava growing regions of Tanzania. The project has been operating in Nigeria since 2020 and has been extended to Tanzania from 2022 up to 2025.

IITA is seeking to recruit a qualified person to fill the vacancy of the **Field Projects Manager** for the **IITA-led IFAD-SSTC and BASICII** projects areas respectively. The position will be for a period of two years renewable subject to availability of funds, a successful probation period and high performance throughout the implementation of the project.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in **Morogoro, Tanzania.**

**Responsibilities:**
- Provide overall leadership and coordination of projects teams to ensure that project targets are achieved within the set timelines and corresponding budgets.
- Develop elaborate work plans for all actions and activities of the projects including preparation of planning, implementation, reporting, monitoring, and evaluation studies.
- For the IFAD-SSTC project, create efficient mechanisms for synergies and extensive sharing of knowledge between the project and the IFAD-funded Agriculture and Fisheries Development Programme (AFDP)
- Managing successful relationships with the government, donor agencies, the business community, related donor-funded projects, and other stakeholders as required.
- Prepare the periodic financial and technical reports which include- quarterly, semi-annual, and annual reports.
- Establish and strengthen productive partnerships with public (district) and private sector partners to facilitate learning and knowledge sharing.
- Organize coordination-planning and review meetings with the project implementing partners
- Work closely with the MEL officer to develop a performance management plan for the projects and monitor the implementation processes to track milestones.
- Ensuring daily management of the projects and assuming full accountability of projects results
- Responsible for day-to-day operational coordination of partner activities,
- Contribute to publication of action research results and success stories.
- Ensuring effective and efficient management of project's compliance with planning, monitoring, evaluation, performance, and reporting
- Work closely with the projects Finance Administrator to ensure monitoring and strict budgetary adherence
- Work closely with the projects Finance Administrator to review and ensure timely submission of regular financial reports
- Perform other activities as may be assigned by supervisor.

**Qualification and Experience**
The candidate should have a master's degree relevant to general agriculture, agribusiness, and seed systems or its equivalent from a recognized university with experience in agricultural technology transfer, marketing, and management of partnerships.

A minimum of five years of senior level field experience in cassava productivity and seed business system

**Core Competencies:**
- Experience of at least 5 years as a project manager/ coordinator of large-scale agricultural development projects, in East Africa and Tanzania in particular.
- Having experience and goo d understanding of production, markets, sustainable seed systems development, marketing challenges and opportunities in Tanzania
- Demonstrated ability to integrate gender, youth, and private sector engagement issues into development projects
- Ability to work collegially and collaboratively in a multidisciplinary and multi-cultural environment.
- Demonstrated communication, networking, computer, and organizational skills and ability to prepare high quality reports.
- Proven experience with engaging with public and private sector stakeholders
- Experience in marketing and business development skills is an added advantage
- Demonstrated ability in stakeholder and partner engagement and policy dialogue with emphasis to district engagement.
- Excellent leadership, interpersonal and team building skills.
- Excellent writing skills.
- Excellent resource mobilization skills

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Morogoro. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.
Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# MAONI & UCHAMBUZI

# Nipashe

## Bravo Tulia, tunatarajia weledi kuongoza Bunge

**BUNGE** limemchagua kwa kura zote 376, Dk. Tulia Ackson kuwa Spika, akijaza nafasi ya Job Ndugai aliyejiuzulu wadhifa huo mapema mwezi uliopita.

Tunampongeza sana Dk. Tulia kwa kuchaguliwa kuongoza moja ya mihimili mitatu inayounda dola na tunamtakia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu hayo mapya.

Hakuna anayeweza kuhoji au kutilia shaka uwezo na weledi, uadilifu wala uzoefu alionao Spika huyo mpya. Hizo ndizo sababu zilizomfanya apitishwe katika ngazi zote za uteuzi, kuanzia Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kamati ya Wabunge wa CCM kisha kuchaguliwa na Bunge zina jana.

Hili linadhihirishwa na Dk. Tulia kupitishwa na Kamati Kuu ya CCM pekee licha ya wanachama zaidi ya 70 kujitokeza kuomba kugombea nafasi hiyo, wengi wakiwa watu wazito na wenye uzoefu wa kutosha.

Kilichodhihirisha zaidi kuwa Spika huyo mwanamke anakubaliwa na wabunge, ni kutokana na jana kumchagua kwa kura zote dhidi ya washindani wake wanane kutoka vyama vya upinzani baada ya kunadi hoja zao mbele ya wabunge.

Mbunge mkongwe kutoka Jimbo la Isimanu, kuliko wote, Willium Lukuvi aliyesimamia uchaguzi huo alimtangaza Dk. Tulia kuwa mshindi kwa kupata kura zote 376 zilizopigwa na wabunge.

Pamoja na pongezi zetu kwake, tunaona kwamba Tulia ana kibarua kikubwa mbele yake kuhakikisha analisimamia Bunge, ambalo mhimili linaundwa na wawakilishi wa wananchi. Majukumu ya Bunge ni kutunga sheria, kufuta sheria zisizofaa pamoja na kuifuatilia na kuisimamia serikali katika utendaji wa shughuli zake za kila siku, zikiwamo wa maendeleo.

Chini ya Dk. Tulia tunatarajia kwamba Bunge halitasita kuhoji 'madudu' ambayo litabaini yamefanywa na watendaji wa serikali ngazi zote (Serikali Kuu) na (Serikali za Mitaa) hususani matumizi ya fedha za walipakodi zinazotumika katika utoaji wa huduma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hatutarajii Bunge kuacha majukumu yake ya msingi ikiwamo kuihoji serikali badala yake kuwa mtetezi na msemaji wake. Kufanya hivyo ni kukiuka maana ya dhana ya mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili yote mitatu ya dola (Serikali, Bunge na Mahakama).

Kilichotia faraja ni hotuba yake fupi baada ya kuchaguliwa alipoeleza nafasi ya Bunge ambalo ni sauti ya wananchi kwamba mhimili huo ni daraja kati ya serikali na wananchi, na kwamba atatumia nguvu zake kuliongoza kwa umakini ili liwe daraja madhubuti kati ya wananchi na serikali na ataliongoza kuishauri serikali ili kutimiza wajibu wake.

Alisema Bunge litauliza maswali na kuhoji serikali kwa hekima na busara, na kuongeza kuwa watafanya hivyo kwa nia thabiti ili wananchi wapate maendeleo.

Katika miaka ya karibuni, zilianza kuibuka hisia na malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu kwamba Bunge limeanza kusahau majukumu yake, hivyo kutojisimamia kama mhimili kamili. Kwa kauli ya Tulia tunatarajia kuona maboresho makubwa katika mhimili huo.


Tusingefurahia kushuhudia minyukano isiyo ya lazima iliyokuwa ikionekana kati ya kiti cha Spika na wabunge wa upinzani na wakati mwingine wabunge wa chama tawala na upinzani.

Lingine tunalomwomba Spika Tulia alifanye ni kurejesha Bunge kuonyeshwa mubashara ili wananchi wasikie yanayojadiliwa na wawakilishi wao katika kuwaletea maendeleo kwenye majimbo yao na taifa kwa ujumla. Hii ndio maana ya kuliita Bunge kuwa ni sauti ya wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wabunge ni utashi wa kisiasa utakaotokomeza ndoa utotoni

Na Sabato Kasika

**TAKWIMU** za mwaka 2010 na 2017 zilizotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto Ulimwenguni (UNICEF), zinaeleza kuwa Tanzania ni ya tatu Afrika kwa kuwa na viwango vya juu vya ndoa za utotoni.

Katika takwimu hizo, Sudani Kusini taifa jipya lililopatikana baada ya kujitenga na Sudan, inakadiriwa kuwa na idadi ya watoto wa chini ya umri wa miaka 18 wanaoozwa ambao ni asilimia 52 ikiwa ni idadi kubwa zaidi, Uganda ina asilimia 40 na Tanzania ni asilimia 31.

Ni mwaka jana kuelekea katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambapo shirika hilo lilitoa takwimu hizo, huku mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayopigania haki za mtoto ukiiomba serikali kufanya marekebisho Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Kuwapo kwa ndoa za utotoni, ni wazi kwamba kunatokana na kutokuwapo kwa usawa wa kijinsia na thamani ya chini wanayopewa wasichana, hali ambayo inachangia kudhoofisha maendeleo ya taifa.

Vita hii inahitaji utashi wa kisiasa kukabiliana na tatizo hilo, hasa kwa wabunge ambao wapo katika nafasi nzuri ya kubuni, kutoa mwongozo ili kutekeleza sheria na sera zinazotakiwa, kupitisha bajeti, kufuatilia utekelezaji na kuhakikisha uwajibikaji unakuwapo.

Wabunge wanaweza kufuatilia na hakikisha sauti za wananchi zinasikika, ikiwa ni pamoja na zile za watoto wa kike. Hivyo, ili kukabiliana na ndoa hizo, utashi na dhamira ya kisiasa ni jambo muhimu.

Kwa nguvu yao kama wawakilishi wa wananchi katika ngazi ya maamuzi, wanaweza kushawishi, kushirikiana na wadau wengine kuelimisha jamii, ili ielewe madhara ya ndoa hizo, hatimaye ibadilike.

Hivyo suala la utashi wa kisiasa ni la muhimu katika kupiga vita ndoa hizo, kwani wawakilishi wa wananchi ndiyo wanaojua hali halisi ya mila na desturi za huko wanakotoka.

Kitendo kilichofanywa na binti ambaye amefaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka huu akajinusuru na kukwepa ndoa ya utotoni, kiwe chachu ya kufuatilia nyendo za wazazi na walezi ambao bado hawajaacha ukatili huo.

Baba mzazi alitaka kumwozesha kwa mahari ya ng'ombe 14, kitendo ambacho binti hakukipenda na kuamua kwenda kutoa taarifa kwa ofisi ya mtendaji wa kata kwa hatua zaidi za kisheria.

Kwa sasa binti huyo amechukuliwa na Shirika la Agape mjini Shinyanga, katika nyumba salama ya watoto wenye madhira ya ndoa za utotoni, kwa ajili ya usalama na anajiandaa kuendelea na masomo ya kidato cha tano.

Inaonekana huyo ameelimishwa na ameelewa umuhimu wa elimu akajinusuru asiingie katika ndoa hiyo ambayo ingekatisha ndoto yake. Je, ni wangapi wenye ushujaa kama binti huyo?

Bado ninaendelea kuamini kuwa wawakilishi wa wananchi kwenye ngazi za maamuzi wakiwamo wabunge, wana nafasi ya kuzunguka katika maeneo yao ya uwakilishi na kuelimisha jamii madhara ya ndoa za utotoni.

Wazazi na walezi pia ni vyema wakatambua kuwa ndoa za utotoni mara nyingi huwa ni mwisho wa fursa ya elimu kwa wasichana. Hivyo ni vyema wakaacha watimize mahitaji yao muhimu na haki zao ikijumuisha elimu.

Lakini ni vyema wakatambua kuwa watoto wa kike wana haki ya kupata elimu na sio wa kuwa mitaji yao kama ambavyo ilitaka kutokea kwa binti huyo aliyekuwa aolewe kwa mahari ya ng'ombe 14.

Jambo lingine ni kwamba, dunia ya leo imebadilika, hivyo kuna haja ya kuachana na mila ambazo zinamkandamiza mtoto wa kike kwa kumgeuza kuwa kitega uchumi kwa kumnyima elimu.

## Mawakili Jamhuri kumhoji Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, leo anatarajiwa kupandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, kuhojiwa na mawakili wa Jamhuri baada ya mawakili wa upande wa utetezi kutumia siku tatu kumwongoza mteja wao.

Sabaya ambaye ni shahidi wa pili wa upande wa utetezi kwa mshtakiwa wa kwanza, anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 27 kwenye mahakama hiyo.

Katika kesi hiyo, mbali na Sabaya washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanaokabiliwa na mashtaka matano yakiwamo ya kuongoza genge la uhalifu, kujihusisha na vitendo vya rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na utakatishaji wa fedha.

Shauri hilo lilisitishwa kuendelea mahakamani huko kwa muda wa siku 10 kupisha shughuli za kimahakama za maadhimisho ya wiki ya sheria.

Hadi sasa kwa mshatiwa wa kwanza (Sabaya), mashahidi wawili wamepanda kizimbani kutoa ushahidi wao akiwamo Mkuu huyo wa zamani wa Wilaya ya Hai na mke wake, Jesca Thomas.

Shahidi wa kwanza wa utetezi, Silivester Nyegu (26), alikamilisha kutoa ushahidi wake mahakamani huko dhidi ya mashtaka yanayowakabili.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu linalowakabili washtakiwa wote, la pili ni kujihusisha na vitendo vya rushwa, likimkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake na la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa linalomkabili mshakiwa wa kwanza peke yake.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linalomkabili Sabaya peke yake na shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linalowakabili washtakiwa wote saba.

# Mtoto adaiwa kuchomwa moto sehemu za siri na mjomba wake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MTOTO wa miaka 10 (jina limehifadhi) katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili (jina la shule linahifadhiwa) amechomwa moto sehemu za siri na mapajani na mjomba wake.

Mkuu wa Dawati la Jinsia, Inspekta Tiho Masatu, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili ofisini kwake kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia.

Alisema kwa sasa matukio hayo yanaongezeka kila siku licha ya kuwapo juhudi mbalimbali za kutokomeza vitendo hivyo.

Masatu alisema tukio hilo la kinyama lilifanywa na mjomba wake ambaye ni mume wa shangazi wa mtoto huyo, aliyejulikana kwa jina la Ramadhani Ali Januari 20, mwaka huu na aligundulika kufanyiwa kitendo hicho na walimu wake.

"Mwendo wake na unyonge aliokuwa nao ndio sababu iliyofanya kumtambua kuwa amechomwa moto na mume wa shangazi yake. Matukio ya kikatili kwa sasa yameongezeka ndani ya jamii, lakini wanafamilia wanashindwa kutoa taarifa,"alisema Masatu. Pia alisema mtoto huyo alichomwa moto kwa kutumia kisu ambacho alikuwa akikiweka katika moto na baada ya kupata moto kumchoma katika sehemu zake za siri na mapajani hali ambayo ilimsababishia maumivu makali na kushindwa kutembea vizuri.

Alisema shangazi wa na mtoto huyo alikuwa akifurahia kitendo alichofanyiwa mtoto huyo na mume wake kwa kuwa hawakutoa taarifa mahali popote juu ya ukatili huo.




Meneja Malipo ya Pensheni wa NSSF, Nancy Mwangamila (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu zoezi la uhakiki wa wastaafu na wategemezi linaloanza. Wengine ni Mameneja Waandamzi wa NSSF, Lulu Mengele (kushoto) na James Oigo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NSSF yaweka utaratibu kuhakiki wastaafu na wategemezi

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umeanza rasmi uhakiki wa wastaafu na wategemezi wanaolipwa pensheni ya kila mwezi, huku ukiwataka walengwa kufika na nyaraka nne muhimu ili kufanikisha zoezi hilo.

Akizungumzia utaratibu wa uhakiki huo ulioanza jana hadi Aprili 29, 2022, Meneja Pensheni wa NSSF, Nancy Mwangamila, alisema mstaafu anatakiwa kufika na nyaraka muhimu ambazo ni kitambulisho cha NSSF au kuponi, kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA, picha moja ndogo ya sasa ya rangi na kwa wategemezi (watoto) wafike na cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha shule.

Nancy alisema Mfuko umeweka utaratibu mzuri kwa wastaafu wagonjwa au wazee wasiojiweza taarifa zao zitolewe kupitia barua pepe customercare@nssf.or.tz au wapige simu ya bure 0800116773 ili waweze kuhudumiwa.

Alisema wastaafu wanaohudumiwa na Mfuko hadi kufikia Desemba 31, 2021 wameongezeka na kufikia 24,894 kutoka 23,164 waliokuwapo mwezi Juni, 2021 sawa na asilimia 7.47.

Alisema idadi ya wastaafu waliopo katika daftari la pensheni ya kila mwezi wanalipwa wastani wa Sh. bilioni 8.4 kwa mwezi.

Nancy alisema lengo la uhakiki huo ni kwa ajili ya kuhuisha taarifa za wastaafu ili kupata sahihi kama sehemu wanazoishi, namba za simu na namba za Kitambulisho cha Taifa.

Alisema kwa wastaafu waliopo Zanzibar watahakikiwa katika ofisi zote za ZSSF zilizopo Unguja na Pemba na waliopo Dar es Salaam uhakiki wao utafanyika katika ofisi za mkoa ambazo ni Ilala, Kinondoni na Temeke pia katika ofisi za wilaya zilizopo Daraja la Mwalimu Nyerere na Mbezi Beach.

Kwa upande wake, Meneja Usimamizi wa Mafao wa NSSF, James Oigo, alisema uhakiki wa wastaafu na wategemezi wanaolipwa pensheni ya kila mwezi ulianza rasmi jana hadi Aprili 29, 2022.

Oigo alisema uhakiki ni muhimu kwa sababu Mfuko unapata taarifa sahihi za wastaafu na wategemezi wake na kuuwezesha kuendelea kulipa mafao kwa wahusika kila mwezi bila ya usumbufu wowote pamoja na kuhuisha kanzi data zake.

Alisema uhakiki utafanyika kila siku Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 10:30 jioni kwenye ofisi zote za NSSF za mikoa na kwamba moja kati ya malengo makuu ya Mfuko ni kutoa mafao ya muda mrefu ambayo ni ya pensheni na mafao ya muda mfupi.

Oigo alifafanua kuwa mafao ya pensheni yanatolewa kwa wanachama waliofikia umri wa kustaafu ambao ni miaka 55 mpaka 59 kustaafu kwa hiari na miaka 60 kustaafu kwa mujibu wa sheria na awe amechangia katika Mfuko michango isiyopungua ya miezi 180 sawa na miaka 15.

Alisema NSSF pia inatoa pensheni ya ulemavu ambayo hulipwa kwa mwanachama aliyepoteza angalau theluthi mbili (2/3) ya uwezo wa kufanyakazi na awe amepata ulemavu wa kimwili au kiakili kama ilivyothibitishwa na taarifa ya daktari na kwamba pensheni nyingine ni ya urithi ambayo hulipwa kwa wategemezi wa mwanachama aliyefariki ambao ni mke/mume na watoto walio na umri usiozidi miaka 18 au 21 ikiwa wapo masomoni.

Oigo alisema katika kuwaondolea usumbufu wastaafu, Mfuko umeunda group la ujumbe mfupi wa maneno (SMS) ambazo zimeshaanza kutumwa kwa wastaafu zikiwataka waende kuhakikiwa kwa vipindi tofauti tofauti kwa mfano baadhi ya wastaafu wataanza kuhakikiwa mwezi huu wa Februari, mwezi Machi na kundi la mwisho mwezi Aprili. Hali itakayoondoa msongamano na kuzingatia tahadhari za ugonjwa wa UKIVO 19.

Aidha, Mfuko katika kuendelea kutoa huduma zake kidigitali umekuwa ukitumia mfumo wa kuchukua alama za kidole gumba (Biomentic/ Fingerprint) utaratibu ambao unarahisisha zoezi la uhakiki na kuwa la muda mfupi kwa kuwa mfumo huo umeunganishwa moja kwa moja na mfumo wa NIDA ambao una taarifa za wanachama na kufanya zoezi la uhakiki kuwa la muda mfupi endapo mstaafu atakuwa na namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA).

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA MIRADI YA UWEKEZAJI WA KIJAMII KWA MAKUNDI YA KIKABILA YANAYOGUSWA NA MRADI WA EACOP**
**KUMBUKUMBU NAMBA. 0010007446**

TotalEnergies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika taasisi (kampuni au AZAKI) zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kubuni na kutekeleza mpango wa uwekezaji wa kijamii kwa makundi ya kikabila yanayoguswa na Mradi.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unatafuta huduma kutoka kwa shirika lenye uzoefu wa kutosha, (Kampuni au AZAKI inaweza kuitikia kwa kuonyesha nia ili kubuni na kutekeleza mipango ya uwekezaji wa kijamii na kujenga uwezo kwa jamii zilizochaguliwa za makundi ya kikabila yaliyoguswa na Mradi katika mikoa ya Tabora, Manyara, Dodoma na Tanga.

Muundo wa programu utalenga kutoa msaada wa uboreshaji wa maisha kimila (wafugaji au wawindaji) wa makundi haya ikijumuisha lakini sio tu usimamizi wa ardhi, afya ya mifugo na ufugaji, mahitaji maalum ya wanawake bali unapaswa kuundwa kwa njia ambayo inazingatia mahitaji ya uhifadhi na uendelevu.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**
Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuleta maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu katika kusaidia makundi ya kikabila yaliyo katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na kubuni na kutoa programu za maendeleo kwa jamii na jumuiya hizo.
- Uthibitisho wa usajili na leseni ya sasa ya biashara kwa makampuni au AZAKI kwa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI).
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kazi data ya EWURA ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha nia ya maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani.

Taasisi yenye nia, ambayo ina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu inapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11 alasiri** saa za Afrika Mashariki (EAT), tarehe **Februari 16 2022 .** Kichwa cha Barua pepe kiwe **0010007446.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni au AZAKI) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taaisi zenye nia. Mwaliko kwa taasisi kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenye vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya UtunzajiwaTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

# Bomba mafuta kuvutia uwekezaji wa trilioni 8/-

**Na Jenifer Gilla**

MAKAMU wa Rais , Dk. Philip Mpango, amesema makadirio ya dola bilioni 3.5 (Sh. trilioni 8,042) yanatarajiwa kupatikana katika uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) katika kipindi cha 2022 na 2025 kupitia mradi wa bomba la mafuta kati ya Uganda na Tanzania.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya kutoa tangazo la uamuzi wa mwisho wa mradi wa uwekezaji wa mafuta kati ya Tanzania na Uganda na kampuni za kimataifa za mafuta, Total Energies ya Ufaransa na CNOOC ya China uliofanyika Kampala, Uganda alikomwakilisha Rais Samia Suluhu.

"Tangazo la leo (jana) ni matokeo ya juhudi kubwa na mazungumzo yasiyokoma kati ya mataifa haya mawili jirani ya Afrika Mashariki, kwa kweli hili ni tukio muhimu," alisema Dk. Mpango.

Kiongozi huyo wa Tanzania alisema mradi huo pia utatoa maelfu ya ajira, takriban ajira 160,000 (zisizo za moja kwa moja) kwa wakazi wa nchi hizo na kuwataka wananchi hao kutumia fursa hiyo kujiingizia kipato.

"Maendeleo yaliyofikiwa kwenye mradi huu tangu ziara yako ya mwisho jijini Dar es Salaam Mheshimiwa Rais (Yoweri Museven) kwa hakika ni ya kuvutia, tunakumbuka jinsi ulivyowasisitiza wabia wetu kumaliza sehemu zilizobaki ili kufikia uamuzi wa uwekezaji haraka, tunafurahi kuona kuwa mradi huu umefikia pale tulipotarajia," alisema.

Rais Museven alisema kuna wasiwasi kwamba mafuta ambayo Uganda inatazamia kuzalisha huenda yasipate soko, akiwaondoa hofu hiyo kwamba hilo halitotokea.

"Tumejifunza hili, hakuna uwezekano wa mafuta hadi kudiba (Kiganda) au kudoda (Kiswahili) - akimaanisha kukosa soko," alisema.

Akitoa tamko la uamuzi wa mwisho wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa TotalEnergies, Patrick Pouyanne, alisema tamko hilo linaashiria dhamira ya kampuni za mafuta kuwekeza zaidi ya dola bilioni 10 katika mradi huo.

"Kwa jina la washirika wa ubia na TotalEnergies, ninatangaza uamuzi wa mwisho wa uwekezaji kwa mradi wa maendeleo wa Ziwa Albert," alisema Patrick. April 11, 2021 Rais Samia na Rais Museveni, walihudhuria hafla ya utiaji saini mkataba kati ya serikali hizo mbili na Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki (EACOP) juu ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la kutoka Hoima, Uganda kwenda Tanga, Tanzania.

Serikali hizo zimekubaliana katika masuala ya hisa, usafirishaji na ushuru katika hatua za awali za mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la mafuta la Afrika Mashariki.

Ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi wa jumla ya kilometa 1,443 kutoka Magharibi mwa Uganda mpaka kwenye Bandari ya Bahari ya Hindi, Tanga.

Ujenzi huo utagharimu dola za Marekani bilioni 3.55 na unatarajiwa kuwa mradi wenye bomba refu zaidi la mafuta duniani.

Mataifa hayo mawili yanatarajia kukuza uchumi na kuzalisha ajira zipatazo 10,000 za moja kwa moja wakati wa ujenzi wa bomba na uendeshaji wa mradi huo huku Uganda ikikadiriwa kutoa mapipa yake ya kwanza ya wastani wa bilioni 1.4 ya mafuta yanayofaa kibiashara mnamo mwaka 2025.

# MCT yaongeza muda tuzo EJAT

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) limeongeza muda wa siku 14 za kupokea kazi za waandishi wa habari wanaowania Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2021.

Vilevile, baraza hilo limeongeza idadi ya vipengele vya kushindanishwa kutoka 19 vya awali hadi 20.

Kwa mujibu wa taarifa yao iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT, Kajubi Mukajanga, kazi hizo zitapokelewa hadi Februari 14, mwaka huu ili kuwapa nafasi waandishi ambao walikuwa hawajawasilisha kazi zao hadi kufikia tarehe iliyokuwa ya mwisho Januari 31, mwaka huu.

"Baraza linawasihi waandishi wa habari ambao awali hawakuleta kazi zao, kuitumia nafasi hii kuziwasilisha. Kuongeza muda kunayahusu makundi yote, nia ya tuzo hizi ni kutambua na kuzienzi kazi bora. Jumla ya makundi 20 yatashindaniwa," alisema.

Alisema baraza limeongeza muda huo kutokana na maombi ya wafadhili kwa makundi ya utawala bora na uwajibikaji na kundi la habari za ushirika ili kutoa nafasi kwa waandishi walioandikia maeneo hayo kuwasilisha kazi zao.

Wakati tuzo hizo zilipozinduliwa Septemba 10 mwaka jana, kulikuwa na vipengele 18, lakini baraza liliongeza kundi moja la kushindaniwa baada ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kutaka kuwapo kwa kundi litakalohusisha habari za vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na shughuli za vyama vya ushirika.

Jana baraza lilitangaza kuongeza kipengele kingine cha habari za utawala bora na uwajibikaji. Makundi mengine yanayoshindaniwa ni: Tuzo ya Uandishi wa Habari za Uchumi, Biashara na Fedha; Michezo na Utamaduni; Kilimo na Biashara; Biashara ya Kilimo; Elimu; Utalii na Uhifadhi; Habari za Uchunguzi; na Uandishi wa Habari za Data.

Mengine ni Haki za Binadamu; Mpigapicha Bora Magazeti; Mpigapicha Bora Runinga; Mchora Katuni Bora; Habari za Jinsia na Watoto; Uandishi wa Habari za Gesi, Mafuta na Uchimbaji wa Madini; Habari za Ulemavu; Afya; Sayansi na Teknolojia; Hedhi Salama; na Kundi la Wazi.

HABARI KITAIFA

# TRA sasa yaja na 'kamata wote'

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imetangaza kuanza kwa kampeni iliyoipa jina la 'Kamata Wote' inayojumisha wauzaji wasiotoa risiti na wanunuzi wasiodai risiti za kielektroniki (EFD) pamoja na kuainisha adhabu watakazotoa kwa wakosaji, zikijumuisha kuwapeleka mahakamani.

Kampeni hiyo ilitangazwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa mamlaka hiyo, Richard Kayombo, alipozungumza na waandishi wa habari kuelekea kuanza kwa kampeni hiyo leo.

Alisema kutotoa risiti na kutodai risiti kunakwamisha juhudi za serikali katika kukusanya kodi ambazo kimsingi pesa hizo huwa zinasaidia kuimarisha huduma za kijamii nchini.

"Kampeni hii ya 'Kamata Wote' inayoanza kesho (leo) itakuwa ni kampeni endelevu na itafanyika nchi nzima, lengo sio kumkandamiza mfanyabiashara ila kujenga utamaduni ili watu watambue umuhimu wa kutoa na kudai risiti pindi yanapofanyika mauziano ya bidhaa.

Pamoja na kwamba watakaokutwa na makosa watapigwa faini na wengine kupelekwa mahakamani, lakini bado zoezi hilo litaambatana na utoaji wa elimu," alisema.

Sanjali na hilo, Kayombo pia alibainisha kuwa wafanyabiashara wanaotakiwa kuwa na mashine za EFD ni wale wote ambao kipato chao kinafikia Sh. milioni 11 kwa mwaka na sio milioni 14 kama ilivyokuwa awali.

Kayombo alitaja adhabu zitakazotolewa kwa muuzaji na mnunuzi pindi watakapobainika na kosa la kutotoa au kudai rositi, akifafanua: "Muuzaji akikutwa na ameuza bidhaa bila kutoa risiti faini yake ni kuanzia Sh. milioni tatu hadi nne na nusu.

"Kama muuzaji unastahili kuwa na mashine ya EFD na hauna pia faini itakuhusu, pili una mashine lakini hutoi risiti, kutoa risiti feki na mwisho kutoa risiti kwa kuchagua watu ukikutwa na makosa hayo yote faini itakuhusu na ikibidi tutampeleka mahakamani na adhabu yake ni kifungo jela miaka mitatu au vyote kwa pamoja."

Kayombo alionya kuwa mteja akinunua bidhaa bila kudai risiti faini yake ni kuanzia Sh. 30,000 hadi Sh. milioni 1.5 lakini makosa mengine yatakayomwingiza katika adhabu ni kukutwa na mzigo ambao haufanani na risiti aliyonayo.

Mkurugenzi huyo pia alikemea tabia ya vishoka kujitokeza na kudai wao ni maofisa kutoka TRA na kuwachukulia pesa wafanyabiashara.

"Tunapotangaza kuanza kwa kampeni kama hizi huwa wanajitokeza makanjanja na kudai kuwa wao ni maofisa kutoka TRA. Kwa hiyo tunaomba wafanyabiashara watakapopata shaka na watu hao watoe taarifa kupitia namba 0800750075, 0800780078, 0744233334," alisema.

Mfanyabiashara kutoka Kituo cha Mafuta kilichoko Bandarini Posta, Jamila Simba, alitaja sababu za baadhi ya wateja kutochukua risiti baada ya kununua mafuta, akisema: "Sisi hapa kituo cha mafuta baadhi ya watu wengi wanaimani potofu utakuta ukishamhudumia mafuta hachukui risiti ukimwambia anadai ni uchafu hana pa kuweka hasa hawa bodaboda ndio wagumu sana kuchukua risiti licha ya kuona risiti imetoka kwenye mashine."

Nipashe pia ilizungumza na muuzaji wa duka la jumla Kariakoo, Inosenti Chuma, ambaye alikiri elimu ya utoaji wa risiti imewafikia kwa kiwango kubwa lakini wengi wao ni wakaidi kufuata utaratibu.

## Ludewa wakunwa kukamilika barabara ya zege kilomita 50

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UJENZI wa barabara ya zege kilomita 50 Lusitu- Mawengi wilayani Ludewa mkoani Njombe, umefikia asilimia 86 kwa kukamilisha zaidi ya km 45 ambapo mradi huo unatarajiwa kukabidhiwa Agosti mwaka huu.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wakazi wa wilaya hiyo walisema barabara hiyo imewarahisishia kusafiri na kusafirisha mazao yao kwani kwa msimu wa mvua walikuwa wakitumia zaidi ya siku moja kutoka wilayani Ludewa hadi mjini Njombe tofauti na sasa ambapo wanatumia saa tatu hadi nne tu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mawengi, Renatho Willa na Aneth Paulo, mkazi wa kijiji hicho ambao wameeleza namna walivyovumilia kwa miaka mingi hadi sasa wamepata barabara hiyo.

"Barabara hii ilikuwa haipitiki kabisa tangu tulipopata uhuru na nauli ilikuwa kubwa sana kwenye vyombo vya usafiri, lakini kwa kilomita ambazo imefikia sasa hivi kweli wananchi wameanza kupata matunda ya uhuru," alisema Lenatho Willa.

Aneth Paulo alisema: "Kuna wakati mwingine utakuta mnakwama huko milimani na kulala pale pale, lakini kwa sasa tunafika Njombe siku moja, kwa kweli tunaishukuru serikali na TANROADS kwa kusimamia ujenzi wa barabara hii," alisema.

Anthony Mtewele, dereva wa mabasi kutoka Ludewa kuelekea mjini Njombe, alisema ujenzi wa barabara hiyo umechukua zaidi ya miaka miwili, alisema hali hiyo ilichelewesha huduma, lakini wanayo furaha kubwa kwa sasa kuona ujenzi unakamilika.

Meneja wa TANROADS mkoa wa Njombe, Lucy Shalua, alisema zimebaki kilomita tano pekee ili mradi ukamilike, huku wakitarajia kukabidhiwa Agosti mwaka huu.

Mhandisi mshauri wa mradi, Dong Moon, alisema atahakikisha mkandarasi, Cheon Kwang, anakamilisha mradi kwa wakati.



Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto (watatu kulia), akikata utepe kuzindua kituo cha kuchakata na kutoa huduma ya majisafi na salama ya kunywa kilichotolewa na kampuni ya Heritage Drinking Water, katika eneo la Gerezani, jijini humo, juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Edwinus Lyaya na (wapili kulia) ni Maneja Masoko wa kampuni hiyo, Sophia Mgala. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## TARURA ilivyojipanga kukabili vikwazo Rufiji

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) Wilaya ya Rufiji, mkoani Pwani imepitisha mapendekezo ya bajeti zaidi ya Sh. bilioni 2.215 kugharamia miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/2023.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Rufiji, Mhandisi Edwin Kabwoto, alitoa taarifa ya mapendekezo ya bajeti hiyo jana katika kikao kilichofanyika Utete wilayani humo kikiwahusisha madiwani na viongozi mbalimbali.

Mhandisi Kabwoto alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 715.29 zitatumika kugharamia kazi mbalimbali za matengenezo ya barabara na Sh. bilioni 1.5 zikitengwa kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Meneja huyo alisema pamoja na mapendekezo ya bajeti, mahitaji halisi ya matengenezo na kufungua barabara ni Sh. bilioni 8.01 kwa kuwa barabara nyingi zinaelezwa kuwa na malimbikizo ya matengenezo, hivyo kuwa katika hali mbaya na kuhitaji fedha kuzirudisha katika ubora.

"Lengo la mpango wa bajeti ya mwaka 2022/2023 ni kuziweka katika kiwango kama iivyo kwa mipango iliyopita na vigezo vimetumika wakati wa utayarishaji kama upatikanaji wa mahitaji ya rasilimali fedha, uwekezaji, watumiaji na aina ya barabara kwa misingi ya madaraja," alisema.

Mhandisi Kabwoto alieleza vikwazo katika idara yake kuwa ni ufinyu wa bajeti, upana wa barabara usiojitosheleza, uwapo wa miundombinu mbalimbali katika barabara zinazojengwa hivyo kusababisha gharama ya kuiondoa kuwa kubwa pamoja na upatikanaji wa vifusi, mawe na kokoto.

Alieleza wamejipanga kukabiliana na vikwazo hivyo ikiwa ni pamoja na kuelimisha na kuomba wadau wa maendeleo ya barabara kama halmashauri kununua mitambo ya kutengeneza barabara kwa ajili ya kuwakodisha makandarasi wanaopata kazi katika wilaya hiyo.

# Nape: TTCL iwe kitovu cha mawasiliano Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amezuru katika Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL - Corporation) na kubainisha kuwa lengo la wizara yake ni kuifanya taasisi hiyo kuwa kitovu cha mawasiliano kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Nape alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam alipozungumza na vyombo vya habari baada ya kutembelea TTCL - Corporation na kuzungumza na menejimenti ya shirika na kupokea taarifa na vikwazo vinavyolikabili.

"Lengo letu ni kuifanya TTCL - Corporation kuwa shirika bora la mawasiliano kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Tunataka tutafute njia ya pamoja ya kuliboresha shirika hili," alisema waziri huyo.

Alisema katika ziara hiyo aliyoiita ya kujifunza, amepokea taarifa ikijumuisha vikwazo vinavyolikabili shirika hilo, akiahidi kuwa wizara inakwenda kukaa na kuvichakata kabla ya kuvitolea maelekezo.

"Tumeyapokea na tunaenda kukaa na kuyachakata, yanayopaswa kufikishwa mamlaka za juu tutayawasilisha na yaliyo chini yetu tunaenda kuyafanyia kazi kisha tutatoa maelekezo yetu ili kusonga mbele.

"Zipo sheria ikiwamo ya ununuzi ya umma, ambazo TTCL imekuwa ikilazimika kuzifuata mchakato wake unaweza kuchukua hadi miezi sita, wakati sekta binafsi ambao ni washindani wa TTCL unaweza hata kuchukua siku mbili... sasa ukimwacha hapo kushindana na wenzake lazima ataachwa mbali," alisema. Waziri Nape alifafanua zaidi akisema kuna baadhi ya mambo ya kiuamuzi ambayo TTCL haiwezi kufanya pekee hadi kushirikisha ngazi nyingine, jambo ambalo limekuwa kikwazo kwenye shirika na kukwamisha baadhi ya mipango ya maendeleo ya shirika.

Aliongeza kuwa amejipanga kukutana pia na wafanyakazi wa TTCL na kuzungumza nao ili kupata maoni na kero zao na kuangalia namna bora ya kushirikiana kuhakikisha shirika linasonga mbele kwa mafanikio zaidi.



Diwani wa Kata ya Kitunda, jijini Dar es Salaam, Victor Vedasto, akizungumza wakati wa ufunguzi wa kambi tiba ya siku tatu ya bila malipo kwenye kituo cha Afya cha One Heaith Polyclinic, kilichopo Bambucha Kitunda Kivule mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Robart Njee na (kulia) ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kerezange, Ismail Abraham. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## RC: Maofisa ugani wawezeshwe mafuta

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAKURUGENZI watendaji wa halmashauri za wilaya mkoani Kagera wametakiwa kuwawezesha mafuta maofisa ugani ngazi ya kata waweze kufikia wananchi na kutoa huduma.

Maelekezo hayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, wakati akipokea pikipiki 12 kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mbuge alisema, mkoa unategemea mafanikio makubwa ya huduma zitakaofanywa na maofisa ugani kwenye maeneo ya wananchi.

"Wizara imetoa pikipkipi ili kuongeza tija na ufanisi kwa kuhudumia na kuwafikia wananchi kusikiliza matatizo yao," alisema Mbuge.

Alisema, mkoa huo una ranchi tano za mifugo zilizoko wilaya za Missenyi, Karagwe, Muleba ambapo kuna maofisa ugani 146 wanohudumia sekta hiyo.

"Tunazo ranchi tano na bado nyingine zipo kwenye taratibu za kuanzishwa hiyo kupanua maeneo ya uwekezaji katika mifugo sasa, nyie wakurugenzi toeni mafuta watu wafanye kazi ikiwezekana ongezeni pikipiki," alisema Mbuge.

Ofisa Mifugo mkoani Kagera, Colman John, alisema, kumekuwapo tatizo la utendaji kazi usioridhisha kwa maofisa ugani ngazi ya kata kwa kutokuwa na usafiri wa kufikia maeneo ya wafugaji.

Alisema kupatikana kwa pikipkipi hizo utasaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuongeza tija inayotegemewa na serikali katika kuboresha kazi zao.

# TWCC yapendekeza mkakati kuboresha mazingira biashara

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

BAADHI ya wanawake wajasiriamali hasa wanaojihusisha na sekta ya kilimo, wametoa mapendekezo ya namna ya kuboresha mazingira yatakayowawezesha kufanya shughuli zao bila kikwazo.

Walitoa mapendekezo hayo kwenye warsha ya kitaifa ya siku mbili mjini Morogoro iliyojadili namna ya kuboresha mpango mkakati wa uboreshaji wa kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara (Blueprint) iliyoandaliwa na taasisi ya uboreshaji mifumo ya masoko kwenye sekta za kilimo ya (AMDT) kwa kushirikiana na Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC).

Paskazia Sebastian kutoka mkoani Kagera, alisema ili kuboresha kilimo hai serikali haina budi kuhakikisha wataalamu wanatoka kwenye viti vyao na kwenda mashambani kuwasaidia wakulima.

Alisema wakitoka na kuwaelekeza wakulima mbinu bora za kilimo hicho kutasaidia kuongeza uzalishaji na tija na hivyo kuweza kuchangia katika pato la taifa.

Aliitaka serikali kuisaidia kwa kuandaa matangazo kuelimisha umma juu ya madhara ya kununua bidhaa za chakula kama asali na mafuta ya kula kutoka kwa wafanyabiashara wa barabarani.

Neema Henjewele aliomba elimu zaidi kutolewa kuhusu mpango mkakati huo wa uboreshaji mazingira ya biashara kwa wananchi wa kawaida kwani wengi wao hawana uelewa wa kutosha.

Alisema kuwa hata yeye alikuwa anausikia tu mpango huo, lakini baada ya kuhudhuria warsha hiyo amekwisha uelewa na sasa atakuwa balozi mzuri.

Aliiomba serikali kuandika sheria mbalimbali kwa kutumia lugha nyepesi na inayoeleweka na jamii ili kuondokana na changamoto mbalimbali. Alisema kuwa lugha nyepesi pia inatakiwa kuandikwa kwenye fomu za maombi ya leseni au usajili wa kitu chochote unaofanyika mtandaoni.

Aidha, waliomba serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kukutana nao na kujadili changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi mara moja.

Walizitaka mamlaka za halmashauri mbalimbali nchini kufanya kazi kwa uwazi kwa kuweka aina ya kodi na tozo kwenye mbao za matangazo.

Akiwasilisha mada, ofisa kutoka Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara, Baraka Eligaesha, aliwataka wajasiriamali hao kutunza kumbukumbu za shughuli zao kwa lengo la kuondo kana na usumbufu usio wa lazima.

Alisema kushindwa kutunza kumbukumbu hizo kunawafanya baadhi ya wajasiriamali waone kama wanaonewa hasa pindi zinapohitajika na hivyo kukaribisha vitendo vya rushwa.

Hata hivyo alisema serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa kufanya marekebisho ya sheria, kanuni na tozo.

Alisema maboresho mengine ni kuunganisha taasisi ambazo majukumu yake yanaingiliana kama Shirika la Viwango (TBS) na TMDA.

"Serikali pia imeweka mifumo ya kielektroniki kwenye kutoa huduma mbali mbali kama leseni, vibali na tozo na kuanzisha vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja ngazi ya halmashauri," alisema.

Akifungua washa hiyo Mwenyekiti wa TWCC, Mercy Silla, aliwataka wajasiriamali hao kuuelewa mpango huo kwani unawahusu katika maisha yao ya kila siku.

Ofisa kutoka AMDT, Tertula Swai, alisema malengo ya warsha hiyo kuwaongezea uelewa wajasiriamali wanawake kuhusu mpango huo.

Karamu mwaka wa 45 CCM kuliwa nyumbani kwao Baba wa Taifa





Ukurasa 13



Ukurasa 14

ROCH CHRISTIAN KABORE

## Amenusurika mapinduzi ya Burkina Faso

siasa

JUMATANO FEBRUARI 2, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

JUMA HAJI DUNI; NGOME YA ACT WAZALENDO

# Ijue milima, mabonde aliyopita na mbigiri zilizomtoboa kisiasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUNA wanaoyataja na kuyafananisha maisha ya kisiasa ya mwanasiasa nguli, na Waziri Kiongozi wa awamu ya tatu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), hayati Maalim Seif Sharif Hamad na Mwenyekiti mpya wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, wakiwaita chanda na pete.

Duni almaarufu "Babu Duni" maisha yake ya kisiasa wakati mwingine yamekuwa yakilinganishwa na ya wanasiasa vigogo katika chama cha ukombozi cha ANC huko Afrika Kusini, walifungwa jela na kuhukumiwa katika kesi za kubambikiwa ili kuwavunja nguvu wasishiriki kwenye harakati za kupinga siasa za kibaguzi .

Pia wapo baadhi wanaoamini na kumtaja moja kwa moja Duni kuwa ndiye kada liyekuwa sahihi na aliyestahili kuwa mrithi halali wa kubeba mikoba na kukikalia kiti cha uongozi wa juu wa ACT Wazalendo kwa wakati huu, baada ya Maalim Seif kufariki.

Duni anatajwa kuwa ni kiongozi anayeweza kuwa kiungo ndani ya chama chake, msikivu, mpatanishi,jasiri na mwanasiasa anayeamini katika maridhiano, uvumilivu na maelewano mwenye shime ya kujenga umoja wa kitaifa pia anayependa kusamehe na kusahau.

Kwa kiasi kikubwa huenda sifa za mwanasiasa huyo ndizo aina ya siasa na uongozi zilizokuwa zikiendeshwa na Maalim Seif na kabla hata hajafukuzwa CCM na hatimaye akasukumwa jela kwa mashtaka ya kukutwa na nyaraka za siri

Ingawaje Duni jina lake halimo kwenye orodha ya wajumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) ya CCM



Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo, Juma Duni Haji. **PICHA: MTANDAO**

enzi ya mfumo wa chama kimoja walioondolewa na sio katika kundi la wanasiasa saba wa CCM waliotimuliwa mwaka 1988, bila kutarajiwa anajiunga na CUF mara tu ilipoanzishwa 1992.

Aidha, jina lake pia halimo kwenye orodha ya wanasiasa walioanzisha CUF wala haonekani kwenye kamati ya mapambano ya kupigania demokrasia Zanzibar chini ya kamati iliyojulikana kama KAMAHURU, iliyokuja kuungana na Chama Cha Wananchi cha Tanzania Bara kilichoongozwa na mkongwe hayati, James Mapalala.

Licha ya kwamba hakuwepo huko, kuingia kwa Duni CUF na kushiriki siasa za chama hicho kabla kundi la Maalim Seif kutimkia ACT Wazalendo 2019 , kulimfanya mwanasiasa huyo kuonekana kuongeza ustawi na nguvu za kuijenga kisiasa CUF, akiwa turufu muhimu katika kuendesha kazi zake kisiasa.

Kama ambavyo Maalim Seif, hakuwamo kwenye orodha ua waasisi wa KAMAHURU wakati huo akiwa kizuizini ," Babu" naye hayumo kwenye orodha ya waanzilishi wa CUF.

Kwa bahati mzuri wanasiasa hao wote wawili "pacha" majina yao yakachomoza na kuwa vinara na tegemeo la kusukuma mbele siasa za upinzani na kusimamia demokrasia kwa mikono yote baada ya ujio wa vyama vingi.

Aidha, anatajwa na wengine kuwa tangu akihudumu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Maalim Seif, alishaweka mizizi na kuwa na kundi kubwa la wafuasi walioamua "kujilipua" wakimuunga mkono mchana kweupe kabla hajafukuzwa CCM na wengine wa-

INAENDELEA UK. 12

JUMA HAJI DUNI; NGOME YA ACT WAZALENDO

# Ijue milima, mabonde aliyopita na mbigiri zilizomtoboa kisiasa




Mwenyekiti mpya wa Chama cha ACT Wazalendo, Juma Duni Haji (katikati) baada ya kutangazwa mshindi katika uchaguzi wa chama hicho jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK. 11**

nadaiwa wakibakia ndani ya SMZ na hata Serikali ya Muungano wa Tanzania.

Miongoni mwa wanasiasa waliojitokeza hadharani kumuunga mkono Maalim Seif kinadharia,tena kwa muda mrefu hata wakiwa SMZ ni Babu Duni. Wanasiasa hao wawili walianza kuzungumzia hatma ya siasa za Zanzibar na Tanzania wakiwa wanasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam .

Duni anakuwa na sifa ya kuwa mtu ambaye lolote analoambiwa na Maalim Seif halibishii, hapingani naye licha ya mara kadhaa kutajwa kuhusika kutaka kusuka uasi, lakini ilipochunguzwa kwa kina haukuweza kupatikana ushahidi hivyo akajiongezea uaminifu mkubwa kwa Maalim Seif.

Wakati sahihi ulipowadia ndipo Duni alipojitokeza hadharani na kuanza kupeperusha bendera ya CUF katika kuendeleza harakati za kisiasa baada ya kumaliza masomo yake ughaibuni na kuamua kurudi rasmi nyumbani .

**MBIO ZA URAIS**

Mwaka 1995 na 2000 Duni anapewa dhamana, akiteuliwa kuwa mgombea mwenza wa urais wa Tanzania, akijiunga na Profesa Ibrahim Lipumba , kutaka kuingoza Serikali ya Muungano. Lakini bila mafanikio. Kwa ujumla Mwenyekiti huyo mpya wa ACT Wazalendo, amekuwa mmoja kati ya washirika waadilifu na wasiri wa Maalim Seif, ndiyo maana mikoba hiyo ya urithi, inamstahili.

Wote wawili pamoja na wanasiasa wengine walishiriki kikamilifu katika juhudi za kusaka upatashi na maridhiano nyakati zote pale hali ya hewa ilipovurugika na wao wakawa bega kwa bega kuwaelekeza wanachama wao wapite kwenye njia ipi sahihi isiyo na makorongo.

> “Amewahi kuwa Mkurugenzi wa Uchumi na Fedha wa CUF, mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010, mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2015.

Kama ilivyoonekana katika maisha ya wanasiasa wengine wa Afrika mfano Mzee Nelson Mandela wa Afrika Kusini, walivyoishi kwa mashauriano na wanasiasa wenzake kama Walter Sisulu, Jacob Zuma na Thabo Mbeki , Duni anapaswa kufuata nyayo za uongozi wa mtangulizi wake huku akifikiria kwanza kujenga umoja na ushirikiano ndani ya ACT-Wazalendo.

Wala hapaswi kubeza au kupuuza chimbuko la migogoro iliyowahi kuwakumba wakiwa CUF hadi ACT Wazalendo na pia haitapendeza ukaonekana mzani wa uongozi wake ukiegemea upande mmoja na kuudharau mwengine.Vinginevyo akienda mchomo au kombo, anaweza kujikuta kuta za chama hicho zikipasuka.

**JINA LA ‘BABU NI SUGU’**

Duni anasifa ya kuitwa mwanasiasa “sugu” aliyekumbana na misukosuko mingi hadi jina lake kuwemo kwenye orodha ya viongozi 18 waliokamatwa, kuwekwa kizuizini miaka mitatu kwa tuhuma ya kula njama na kutaka kuipundua Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Wapo wanasiasa wengi ndani ya ACT Wazalendo kutoka CUF ambao wametoka mbali na CUF kuelekea ACT- Wazalendo , baadhi wamehama , hivyo analazimila kukumbuka migawanyiko iliyowahi kutokea na baadhi ya viongozi na wanachama waliohama na kuanzisha FORD na ADC .

Utayari wake,umadhubuti na uongozi wake ndiyo msingi wa chama hicho chini ya unahodha wake, kukisaidia kubaki salama,kuendelea kulipandisha tanga, kutweka , kukata mawimbi na kutia nanga kwenye bandari yoyote ,yeye na abiria wake wakifika salama bila misukosuko ambako ndiko kufanikisha demokrasia.

Maelewano na ukaribu wa Duni na Maalim Seif unatajwa ni mkubwa na mara kadhaa mwanasiasa huyo aliyekuwa ni bosi wake kisiasa huku akiteuliwa kushika nyadhifa kadhaa nyeti ndani ya CUF. Hata pale kundi la baadhi ya wanaCUF walipoamua kuhamia ACT, Duni akawa Makamu Mwenyekiti.

**MAISHA YA UONGOZI**

Baadhi ya nyadhifa alizowahi kushika akiwa CUF ni pamoja na Naibu Katibu Mkuu CUF Zanzibar, Mkurugenzi wa Uchumi na Fedha, Makamu Mwenyekiti na mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi .

Mwenyekiti huyo mpya wa ACT - Wazalendo pia anaonekana kuanza harakati za kisiasa tangu akiwa anasoma Sekondari ya Gamal Abdel Nasser kisiwani unguja alipochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Vijana wa Chama cha Afro Shiriza Party (ASP).

Duni ni wazi anakabiliwa na kibarua kizito cha kukiongoza chama cha ACT - Wazalendo ambacho kimeongozwa na mwanasiasa mashuhuri Maalim Seif na kufanikiwa kukibakiza kwenye uso ule ule ulioachwa na mtangulizi wake.

Anatakiwa awe kiongozi anayezipima siasa za visiwa vya Unguja na Pemba, atakayezilea lakini pia atakayeendesha vyama na mapambano ya nguvu ya hoja badala ya siasa za mti kwa macho ambazo sasa zimeanza kutoweka baada ya kutandikwa zulia jipya la maelewano .

**WASIFU WA DUNI**

Juma Duni mrithi wa Maalim Seif kwa nafasi ya uenyekiti ACT -Wazalendo, amezaliwa Novemba 26, 1950, Zanzibar na ni baba mwenye ndoa, aliyesoma Chuo Kikuu cha Manchester Uingereza na kupata shahada ya uzamili ya Rasilimali Watu mwaka 1994-1995.

Pia amehitimu ngazi ya Post Graduate Diploma ya Biashara, mwaka 1993-1994 pia ni mtaalamu wa Mipango ya Kiuchumi akisomea nchini Japan mwaka 1982.

Amesoma Nigeria mwaka 1980 na pia ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alikosoma Shahada ya Sayansi na Ualimu (Bsc Education) mwaka 1972- hadi 1975.

**UZOEFU WAKE KIKAZI**

Aliwahi kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, 1981-1982. Aidha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda mwaka 1980 -1981, amekuwa mjumbe wa Bodi mbali mbali kama Shirika la Uchumi na Uzalishaji la CCM SUKITA, Ofisa Mipango Elimu na mwalimu wa sekondari.

Kwenye shughuli za kisiasa amekuwa Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo -Taifa kuanzia Machi, 2020 hadi Oktoba, 2021. Aidha amewewahi kuwa Naibu Kiongozi wa chama hicho .

Amekuwa Waziri wa Afya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar kuanzia mwaka 2012 hadi 2015. Duni aliwahi kuwa mjumbe wa kamati mbalimbali za kitaifa, ikiwamo ya Mazungumzo ya Muafaka na Maridhiano ya Kisiasa Zanzibar. Aidha mjumbe kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuanzia 2010 hadi 2015.

Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi Taifa CUF, Naibu Katibu Mkuu CUF (Zanzibar), kati ya mwaka 1999 hadi 2010 amekuwa mjumbe Baraza la Wawakilishi wa Kuteuliwa.

Amewahi kuwa Mkurugenzi wa Uchumi na Fedha wa CUF, mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010, mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2015.

**KUFUNGWA KISIASA**

Duni amewahi kuwa mfungwa wa kisiasa kwa kesi iliyodaiwa kuwa ya uhaini kwa SMZ mwaka 1997 hadi 2000, lakini pia amewahi kuwa mfungwa wa kisiasa kwa kesi ya madai ya kuuwa askari polisi aliyeuwawa Pemba kati ya mwaka 2001-2002.

# Karamu mwaka wa 45 CCM kuliwa nyumbani kwao Baba wa Taifa

Na Beatrice Shayo

CCM iliyozaliwa Februari 5, mwaka 1977 inatimiza miaka 45 Jumamosi wiki hii na maadhimisho ya jubilii hiyo yanafanyika mkoani Mara, alipozaliwa mwasisi wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Chama hicho ambacho ni muungano wa vyama vya ukombozi, Afro Shiraz Party (ASP) na Tanganyika African National Union (TANU), kilizaliwa rasmi kwenye Uwanja wa Amani visiwani Zanzibar , Februari 5, 1977.

Chama kinajinasibu kuwa na historia iliyotukuka hivyo kuwa na kila sababu ya kuadhimisha na kusherehekea siku hiyo adhimu, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, anasema.

Anaongeza kuwa kilele cha maadhimisho mwaka huu wa 45 ni mkoani mkoani Mara katika mkoa alikozaliwa Baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Nyerere na mgeni rasmi atakuwa Mwenyekiti wa CCM Rais Samia Suluhu Hassan.

"CCM imara shiriki uchaguzi kwa uadilifu. Ni kauli mbiu ya maadhimisho haya" anasema Chongolo.

Akizungumzia maadhimisho hayo ya miaka 45 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi anasema wanaCCM wote wanajivunia mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa na chama chao.

Anawaambia kuwa chama kimeendelea kuaminiwa na umma wa Watanzania na kupewa dhamana kupitia sanduku la kura, hivyo kukabidhiwa ridhaa ya kuunda serikali, kushika na kuongoza dola kwa miongo kadhaa.

"CCM imeendelea kusimamia kuwepo kwa mazingira na fursa za Watanzania kujipatia maendeleo katika nyanja zote zikiwamo, afya, elimu, miundombinu ya barabara, reli, anga, mawasiliano, kilimo, nishati, ukuaji wa masoko kwa mazao ya biashara, uvuvi, ukuzaji na ustawi wa diplomasia ya kiuchumi na ushirikiano wa kimataifa,"anasema.

Anaongeza kuwa miaka 45 ya CCM ni ya kujivunia kulinda na kudumisha uhuru wa nchi na raia wake, kuendelea kusimamia Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

Anasema hizo ni mojawapo ya tunu za Watanzania, kusimamia ujenzi wa taifa na kuwaunganisha kwa tamaduni zao tofauti, huku taifa likienzi na kudumisha amani na utulivu.

Anasema CCM imeendelea kusimamia haki na maendeleo ya wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara na wananchi wengine kwenye shughuli halali za uzalishaji mali.

Aidha, Chongolo anasema miaka 45 ya CCM, nchi inajivunia kujitawala na kuongozwa kwa misingi ya kijamaa na kidemokrasia.

"Chama kimeendeleza mapambano dhidi ya maadui watatu umaskini, ujinga na maradhi, kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Watanzania," anaongeza Katibu Mkuu wa CCM.

Anasema katika mapambano ya kujenga taifa chama kimeendelea kuongoza jamii inayozingatia usawa kwa raia wote, bila kujali jinsi, rangi, kabila, dini au hali ya mtu na kusimamia ukomeshaji wa vitendo vyote vya dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu na upendeleo miongoni mwa Watanzania.

Anapongeza juhudi za kushirikiana vyema na vyama vingine vya Afrika na duniani, kwa madhumuni ya kuleta umoja wa bara zima pamoja na duniani pia.

Anasema wakati vyama viwili vya ukombozi vya ASP na TANU, vinaungana idadi ya wanachama ilikuwa ni ndogo, lakini sasa CCM ina wanachama takribani milioni 15, wenye kadi na wanaolipa ada za uanachama, hao ni mbali na wakereketwa na wapenzi wake.

Anaeleza kuwa mwaka huu wamedumisha na kuendeleza matembezi ya mshikamano na kutoa fomu kwa wanachamama, wakereketwa na wananchi wa mikoa yote 32, kumuunga mkono Rais Samia kwa lengo la kuchangia fedha kugharamia kadi za kielektroniki za chama. Anakumbusha kuwa kazi ya uzinduzi wa kadi hizo inatarajiwa kufanyika Februari 5 wakati wa maadhimisho hayo ya jubilii ya miaka 45.




Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

> Kwa kutambua uimara wa CCM mashina na matawi yake, chama kimeendelea kusimamia utekelezaji wa kukagua na kuimarisha uhai na demokrasia mashinani na matawini.

### CCM NA MAGEUZI

Chongolo anazungumzia chama kupitia mageuzi mbalimbali tangu kilipozaliwa miaka 45 iliyopita ili kiendane na nyakati na hiyo ndiyo siri ya uimara wa chama hicho.

Anasema mwaka 1981 CCM ilifanya mageuzi na kujitathmini kifikra na kutoa mwongozo wa CCM wa mwaka 1981 ambao kwa ujumla ulibeba fikra za kujikosoa na kukosoana kuwa ni silaha ya uanamapinduzi.

"Mwongozo huo ulikifanya chama kuzalisha fikra mpya na kuruhusu mawazo mapya. Ilipofika 1992, kiliongoza na kusimamia, kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi licha ya wananchi wengi kutokuukubali."

Aidha, anataja mabadiliko ya muundo wa kiuongozi ya kutoka katika wajumbe wa kamati kuu wa kuteuliwa na kukubali kuingiza wajumbe wa kuchaguliwa.

Anasema CCM ilikubali na kusimamia mageuzi ya uendeshaji wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuufanya kuwa ni uongozi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

### MADHUMUNI YA MAADHIMISHO

Chongolo anasema maadhimisho ya miaka 45 ya CCM mwaka huu, yanalenga kutoa uelekeo wa masuala ya msingi ya chama katika kusimamia kwa ufanisi zaidi malengo makuu ya mradi wa awamu ya nne wa kujenga na kuimarisha chama, hasa ukizingatia mwaka huu ni wa uchaguzi mkuu ndani ya chama.

Chongolo anasema kuna baadhi ya masuala yanayoendelea kushughulikiwa kama yalivyoelekezwa katika mkutano mkuu wa tisa wa CCM wa Taifa, ambayo ni kuongeza idadi ya wanachama na kuwahamasisha kulipa ada kwa wakati na kufanya usajili wa wanachama na jumuiya kwa mfumo wa kielektroniki pamoja na kutoa kadi za kielektroniki kuwa endelevu.

"Kusimamia kwa ufanisi kazi za utambuzi, usajili, uhifadhi, na udhibiti wa taarifa za mali na rasilimali za chama na jumuiya zake kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na kusimamia utekelezaji wa sera ya CCM ya kujitegemea kimapato na kiuchumi ya mwaka 2014,"anasema.

Anaongeza, "kwa kutambua uimara wa CCM mashina na matawi yake, chama kimeendelea kusimamia utekelezaji wa kukagua na kuimarisha uhai na demokrasia mashinani na matawini."

Anasema wataendelea kuhakikisha CCM inakuwa kiungo na daraja linalowaunganisha wananchi na serikali, na kuyatangaza mafanikio ya serikali mbili, kuendeleza na kukuza demokrasia ndani ya chama na jumuiya zake na kudumisha Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 964 yaliyoleta uhuru.

Anasema wataendeleza utafiti, kuimarisha utendaji wa vyombo vya habari vya chama ili kubuni mbinu mpya ya kueneza hamasa, kuenzi utamaduni wa kitaifa na kuboresha njia za mawasiliano kwa umma.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Christian Kabore; aliyeng'oka madarakani Burkina Faso

• Arithiwa rasmi na 'mjeshi' Paul Damiba

**Na Christina Mwakangale**

BURKINA FASO sasa inaongozwa na jeshi, baada ya maofisa wake kutangaza kuelekea mwishoni mwa mwezi uliopita kuwa wamemtumbua Rais Roch Christian Kabore na kutwaa serikali.

Tangazo linatolewa katika televisheni ya taifa na likisema serikali na bunge vimevunjwa na sasa wenye 'kombati' ndiyo wanaoongoza nchi.

Mahali alipo rais huyo hapafahamiki ingiwa shirika la habari la AFP lilinukuu vyanzo vya usalama vikisema kuwa Kabore na mawaziri wengine wako katika kambi ya Sangoule Lamizana iliyo katika mji mkuu wa n chi hiyo .

Siku tatu zilizopita , Luteni Kanali Paul-Henri Damiba, aliyeongoza mapinduzi hayo ya kumtumbua Roch Kabore, anajitokeza hadharani kwenye vyombo vya habari.

Anaanza kwa kumlaumu Kabore kwa kushindwa kuleta amani nchini humo na kukabiliana na vikosi vya wanamgambo wa Kiislam.

Hata hivyo hakujawa na mawasiliano kutoka kwa Rais Kabore mwenyewe tangu alipopinduliwa, hapo awali alituma ujumbe kwenye mitandao ya kijamii akipongeza timu ya taifa ya kandanda ya Burkina Faso kwa ushindi wao katika mechi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) yanayoendelea nchini Cameron. Burkina Faso imeingia kwenye robo fainali za kombe hilo.

### HISTORIA YA KABORE

Kabore amekuwa Waziri Mkuu wa Burkina Faso kati ya 1994 na 1996. Kadhalika alikuwa Rais wa Bunge Dogo la Burkina Faso kuanzia mwaka 2002 hadi 2012.

Wakati huo huo amekiongoza chama cha Congress for Democracy and Progress (CDP) , hadi mwaka 2014 alipoondoka.

Kabore, ambaye ni mtoto wa mtumishi wa umma, baba yake ni Charles Bila Kabore, ambaye aliwahi kuwa waziri wakati wa uongozi wa Rais Maurice Yameogo, huyu alikuwa Rais wa kwanza wa Burkina Faso ambayo wakati huo ilikuwa ikiitwa Upper Volta, akiliongoza taifa hilo kuanzia mwaka 1959 hadi 1966.

Rais huyo wa sasa aliyetumbuliwa na jeshi kitaaluma ni mbobezi wa masuala ya benki na alikuwa mtumishi wa benki ya The International Bank of Burkina (BIB).

Hakuanza kazi leo , alifanya kazi pamoja na Rais Thomas Sankara, aliyeuawa mwaka 1987, na wakati huo alipandishwa cheo na kuwa mkuu wa benki ya BIB ambayo kipindi cha uongozi wake ilikuwa benki kubwa na yenye mtandao karibu nchi nzima.

### AWAMU ZA MAPINDUZI

Burkina Faso ambayo awali ilijulikana kama Upper Volta, ni taifa lenye mzizi wa uongozi kupitia mapinduzi.

Rais wa kwanza wa Upper Volta, alikuwa Maurice Yamego, alifuatiwa na Aboubakar Sangoulé Lamizana, wengine ni pamoja na Thomas Isidore Sankara, akifuatiwa na Blaise Compaore, aliyeiongoza nchi hiyo kuanzia 1987 hadi 2014.



Roch Christian Kabore. **PICHAZOTE: MTANDAO**



Paul-Henri Damiba

> Kabore alipinduliwa Januari 24 na kabla ya hapo wanajeshi waasi walitaka kuachishwa kazi kwa maofisa wa jeshi na kuongeza rasilimali za kukabiliana na wapiganaji wa Kiislamu.

Mwingine ni Gilbert Diendéré, aliyepindua nchi na kushika uongozi mwaka 2015. Diendere alirithiwa na Roch Christian Kaboré, ambaye ameangushwa na Paul-Henry Damiba. Kabla ya mapinduzi hayo, wanajeshi walidhibiti kambi za jeshi, milio ya risasi ilirindima katika mji mkuu wa Ouagadougou, huku chama tawala cha Peoples Movement (PMP), kikisema kwamba, Kabore, waziri wake wamenusurika katika jaribio la kuuawa.

Kabore alipinduliwa Januari 24 na kabla ya hapo wanajeshi waasi walitaka kuachishwa kazi kwa maofisa wa jeshi na kuongeza rasilimali za kukabiliana na wapiganaji wa Kiislamu.

Taarifa ilitolewa na kundi ambalo halivumi sana lenye, vuguvugu la the Patriotic for Safeguard and Restoration - MPSR, kifupi chake kwa lugha ya Kifaransa, linalojumuisha vitengo vyote vya jeshi, imeamua kusitisha wadhifa wa Rais Kabore leo," ilisema taarifa hiyo.

Kabla ya tangazo hilo, Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Uchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS), waliyalaani mapinduzi hayo, wakieleza kwamba wanajeshi watawajibika kwenye usalama wa Kaboré, iwapo lolote litatokea.

Picha ya video kutoka mji mkuu zilionyesha magari ya kivita, yaliyotelekezwa mtaani, yaliyodaiwa yalikuwa na mashimo ya risasi.

Mamia ya raia wamejitokeza kuwaunga mkono wanajeshi hao na baadhi yao walichoma moto makao makuu ya chama tawala. Amri ya kutotoka nje wakati wa usiku imetangazwa.

### SABABU YA MAPINDUZI

Mapinduzi hayo, kwa Burikana Faso si kitu kigeni kwa nchi za Afrika Magharibi jeshi kufikia hatua hiyo, kwani nchi jirani yake,miezi michache yamefanyika mapinduzi.

Mapinduzi ya kijeshi nchini Burkina Faso hayajapokelewa vyema, ingawa sio jambo ambalo halikutarajiwa.

Kuondolewa madarakani kwa Rais Roch Kaboré ni mapinduzi ya nne Afrika Magharibi ndani ya mwaka mmoja na nusu uliopita. Nchi jirani ya Mali, imeshuhudia mapinduzi ya kijeshi mara mbili katika kipindi hicho, yakichochewa na wasiwasi juu ya kushindwa kukabiliana na ongezeko la ghasia za wanamgambo wa Kiislamu.

Kama ilivyokua Mali, kuondolewa kwa Rais Kaboré, kulichochewa na hali ya kutoridhika miongoni mwa vikosi vya usalama kwa madai ya kutoungwa mkono kikamilifu dhidi ya wanamgambo wanaohusishwa na Al-Qaeda na kundi la Islamic State (IS).

Kuliripotiwa matukio kadhaa, kwenye kambi kadhaa za kijeshi, katika mji mkuu, Ouagadougou na miji ya kaskazini ya Kaya na Ouahigouya. Machafuko hayo yalifuatia miezi kadhaa ya maandamano dhidi ya serikali ya kumtaka rais huyo aondoke.

Mashambulizi ya wanamgambo yaliyoanza mwaka 2015 yamesababisha vifo vya zaidi ya watu 2,000 na kuwalazimisha milioni 1.5 kuyahama makazi yao, kwa mujibu wa makadirio ya Umoja wa Mataifa (UN). Imani ya umma katika usimamizi wa rais wa mzozo wa usalama, ilishuka sana baada ya shambulio katika kijiji cha kaskazini cha Solhan, Juni mwaka jana.

Zaidi ya watu 100 waliuawa katika shambulio linalodaiwa kutekelezwa na wanamgambo waliovuka na kuingia nchini humo kutoka Mali.

### MTINDO WA MAPINDUZI

Licha ya hali tete ya kiusalama na kisiasa ya Afrika Magharibi, Burkina Faso ilifurahia utulivu uliodorora hadi uasi wa watu mwaka 2014 ambao ulimwondoa madarakani aliyekuwa Rais wa muda mrefu, Blaise Compaoré.

Mtindo wa majaribio ya mapinduzi yapo tangu mwaka 2015, ambayo yalisababisha mgawanyiko mkubwa ndani ya jeshi. Kaboré alichaguliwa mara ya kwanza mwaka huo kwa ahadi ya kuunganisha nchi.

Hata hivyo, wanamgambo kutoka nchi jirani ya Mali, ambako waasi waliotaka kujitenga mwaka wa 2012 walitekwa nyara na wanajihadi, walifanya shambulio katika mji mkuu wa Burkinabè huku Kaboré akijiandaa kuchukua usukani.

Makundi yenye silaha yalichukua fursa ya uwepo dhaifu wa usalama katika maeneo ya mipakani ya Burkina Faso ili kuendeleza mashambulizi zaidi na kuimarisha uwepo wao ambao wengi ni wanajihadi pia wamezusha mvutano wa kimadhehebu kati ya jumuiya za Kikristo na Kiislamu, zilizokuwapo hapo awali, Burkina Faso.



# DC azuia kesi za ukatili kwenye mabaraza ya vijiji

**Na Renatha Msungu,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Munkunda, amewaagiza wenyeviti wa vijiji kuhakikisha kesi za ukatili na nyingine zipekekwe mahakamani badala ya kusikiliza katika mabaraza ya kijiji.

Munkunda aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa Mahakama ya Wilaya ya Bahi uliofanyika juzi jijini Dodoma.

Alisema imekuwa kama desturi ya watu wa vijijini kuamua kesi wao wenyewe ambapo alisema hivi sasa hataki kusikia suala hilo kwa sababu mahakama ziko na zina mahakimu wanaofanya kazi yao ipasavyo.

"Nawaomba mwelewe nyie wenyeviti wa vijiji hakikisheni kesi zinazohusu makahama zinapekekwa mahakamani," alisema Munkunda.

Alisema bàdo kuna changamoto ya uwepo wa Mahakama za Mwanzo katika wilaya hiyo hivyo amemwomba Jaji Kiongozi wa Mahakama nchini kuwaongezea mahakimu kwa ajili ya kufanya kazi ya utoaji haki kwa wananchi.

Alisema baadhi ya maeneo watu wanasafiri kilomita 120 kufika Makao Makuu ya Wilaya kwa ajili ya kusikiliza kesi zao.

Alisema wilaya hiyo ina kata 22 ina mahakama mbili zinazofanya kazi na moja haitumiki hivyo bado wanahitaji mahakama zaidi za kuwasaidia kutoa haki na kutatua migogoro ya wananchi.

"Uwepo wa jengo hili utarahisisha kazi za usimamizi wa shughuli za serikali ndani ya Wilaya ya Bahi," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema Tanzania ina jumla ya kata 3,956 lakini ni kata 960 ndizo zenye mahakama.

Kwa upande wake Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Mustapha Siyani, aliwataka wananchi kutumia mahakama kutafuta haki.

"Malengo vya ujenzi wa mahakama hii ya kisasa hayatakuwa na matokeo chanya kama wananchi hawataitumia mahakama ili kupata haki wanayostahili," alisema Jaji Siyani.

Alisema maboresho yanayoendelea kwenye mahakama yanakwenda sambamba na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayotambua na kuelekeza maboresho katika taasisi zote za umma kwa kuweka mikakati, miundo na mifumo itakayoimarisha uwazi na uwajibikaji.

Alisema katika utekelezaji wa malengo hayo ndio msingi wa nguzo ya tatu ya mpango mkakati wa mahakama wa miaka mitano (2015/2016-2020/2021) na sasa 2020/2021-2024/2025) uliojikita katika kujenga imani ya wananchi kwa mahakama na ushirikishwaji wa wadau msisitizo ukiwa katika kuzingatia uadilifu katika utendaji wa kazi.

Alisema katika tafiti za hivi karibuni tathmini iliyofanyika katika kipindi cha miezi 12, watumiaji wa huduma ya mahakama waliridhishwa na huduma za mahakama kwa asilimia 64, kulingana na utafiti wa mwaka 2015

ambapo takwimu kuhusiana na huduma kwa mteja ilipanda hadi kufikia asilimia 79 mwaka 2019.

Alisema kwa upande wa maadili ya kazi, katika utafiti wa mwaka 2019, asilimia 83 ya watumiaji wa huduma za mahakama walionyesha kuridhika

na maadili ya watumishi wa mahakama katika utendaji wao wa kazi ikilinganishwa na asilimia 62 kwa utafiti wa mwaka 2015.

## Mfumo mpya uuzaji kahawa Kagera sasa kuanza mwezi huu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema kuanzia mwezi huu, kutakuwa na mfumo mpya wa kuuza kahawa kwa wakulima wa Mkoa wa Kagera.

Akizungumza juzi wakati wa mkutano uliowakutanisha waigizaji na wasambazaji wa mbole, alisema mfumo huo utakuwa mkombozi kwa wakulima wa mkoa huo.

Alisema kutakuwa na mfumo mpya wa kuuza kahawa tofauti na ule wa zamani ambao mkulima alijikuta na tozo karibu 50.

"Tunakuja na mfumo mpya wa uuzaji wa kahawa ambao utawanufaisha wakulima wa Kagera, huko nyuma kulikuwa na mfumo wa ovyo katika uuzaji wa kahawa," alisema.

Alisema kulikuwa na tabia ya kuuza kahawa mbichi ikiwa bàdo shambani (butura).

"Butura kuuza kahawa mbichi ikiwa shambani na mkulima husubiri miezi mitatu ili kulipwa fedha zake hauna manufaa yoyote kwa wakulima," alisema.

Alisema mfumo wa kuuza ndizi na kahawa unafanya wanashindwa kufikiria mfumo mwingine wowote zaidi ya huo.

Pia alisema kuna masoko ya mipakani ikiwamo Kyerwa Kagera na Uganda wakulima wanaweza kuwekewa utaratibu mzuri wa kufanya biashara na Uganda kutokana na uwapo wa ndizi nyingi zinazozalishwa ambazo huitaji masoko.

Aidha, waziri huyo alisisitiza wananchi wenye akiba ya chakula kutunza chakula chao vizuri sambamba na kutumia vizuri mvua zinazonyesha. Alisema nchi ina akiba ya tani 200,000 za chakula.

"Kwa baadhi ya maeneo mvua zinanyesha ni vyema wakulima wakatumia mvua hizo vizuri," alisema.

Mkoa wa Kagera ni moja ya mikoa inayozalisha kahawa kwa wingi ambapo wastani wa uzalishaji wa kahawa ya maganda kwa mwaka ni tani 50,000, kwa mujibu wa takwimu za uzalishaji kahawa kitaifa.



Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Mbelle James, akizungumza na wataalamu wa afya kuhusu umuhimu wa kujifunza lugha ya alama kwenye mafunzo yaliyoandaliwa na mradi wa kuhamasisha utolewaji wa huduma shirikishi za afya kwa watu wenye ulemavu, jijini Dodoma jana, unaofadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society kwa kushirikiana na Kanisa la Viziwi la Betheli Baptisti Tanzania (KVBBT). **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaombwa mkazo lugha ya alama

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuweka mkazo wa matumizi ya lugha ya alama katika taasisi zake za kutolea huduma mbalimbali za umma, ikiwamo kwenye vituo binafsi, hospitali, vituo vya afya, polisi na vinginevyo ili watu wasiosikia wahudumiwe ipasavyo na kwa uhakika.

Hatua hiyo ya kuweka mkazo itawawezesha watumishi kupewa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya lugha ya alama na kuwahudumia watu wenye ulemavu wasiosikia viziwi kulingana na mahitaji yao.

Ushauri huo umetolewa na mradi wa kuhamasisha utolewaji wa huduma shirikishi za afya kwa watu wenye ulemavu katika Jiji la Dodoma unaofadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society kwa kushirikiana na Bethel Baptist Deat Church of Tanzania.

Akizungumza kwenye mafunzo yaliyowashirikisha wataalamu wa afya kutoka vituo vya afya jiji la Dodoma, Katibu wa CHAWATA mkoa wa Dodoma, Mchungaji Kalebi Mhawi, alisema kuwa matumizi ya lugha ya alama itawawezesha wataalamu kuwahudumia ipasavyo.

Alisema kuwa serikali na taasisi zake zikiwamo hospitali, zinatakiwa kushirikiana na vyama vya asasi za viziwi zenye ujuzi na uzoefu wa masuala mbalimbali ya kitaaluma na maendeleo.

"Hivyo basi ni vema serikali kupitia Wizara ya Afya ikachukuwa hatua za haraka kuwaandaa wataalamu wa lugha ya alama na kusambaza katika sehemu za kutolea huduma ya afya, ili kuwezesha viziwi wanapokwenda kutafuta huduma wasikumbane na vikwanzo," Mhawi alisema.

Mratibu wa mradi huo wa kuhamasisha utolewaji wa huduma shirikishi za afya kwa watu wenye ulemavu katika Jiji la Dodoma, Askofu Mkuu wa Kanisa la Bethel Baptis Deaf Church of Tanzania, Frank Sarungi,

alisema bado kuna changamoto kwa watu wenye ulemavu wasiosikia kupata huduma mbalimbali zinazokidhi vigezo vya afya, kutokana na wataalamu wao kutokuwa na uelewa wa elimu ya lugha ya alama.

Alisema kuwa kutokana na kukosa uelewa huo wa lugha ya alama ni vema sasa serikali ikachukua hatua ya kuwawezesha wataalamu wa afya hao wajifunze ili wawe sehemu ya rafiki ambao watakaoweza kuwahudumia ipasavyo. Naye Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Mbelle James, alisema kuwa bado kuna ugumu wa mawasiliano kati ya watoa huduma za afya na watu wenye ulemavu wa kutosikia katika kuwahudumia, hivyo ni wakati sasa wa kuchukua hatua ya kuwawezesha wataalamu hao mafunzo ya lugha ya alama.

Dk. James alisema kutokana na ugumu huo amewataka watoa huduma ngazi mbalimbali za afya kujifunza lugha za alama ili waweze kuwahudumia watu wenye ulemavu kulingana na mahitaji yao.





# Waliotumbuliwa waitunishia misuli CHADEMA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya Kamati Tendaji ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuwatumbua viongozi wote wa chama hicho Wilaya ya Mbeya Mjini, viongozi hao wamesema hawatambui uamuzi huo wa viongozi wa kanda, hivyo bado ni viongozi na wataendelea kutumikia nafasi zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mbeya Mjini, John Mwambigija maarufu kwa jina la Mzee wa Upako, alisema uamuzi uliofanywa na Kamati Tendaji ya Kanda ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mchungaji Peter Msigwa haukuwa sahihi.

Alisema viongozi hao walifanya uamuzi bila kuzingatia Katiba ya chama hicho na kwamba kwa mujibu wa Katiba hiyo, viongozi hao hawana mamlaka ya kumwondoa yeye pamoja na wajumbe wake kwenye nafasi walizochaguliwa na wanachama.

Alisema wanaendelea kutekeleza majukumu ya chama ikiwamo kuandikisha wanachama kwa mfumo wa digitali pamoja na ujenzi wa ofisi ya chama ngazi ya jimbo ambayo alisema tayari mipango imekamilika.

Alisema wameunda kamati mbalimbali za ujenzi ambazo zinaendelea na mikakati ya kuhakikisha ujenzi huo unafanikiwa.

"Msigwa na wenzake wanne ama watatu hawana mamlaka kwa mujibu wa Katiba ya CHADEMA kutuvua uongozi sisi, Kamati Tendaji ya Chama Kanda ina wajumbe 10, lakini waliokuwapo na kufanya maamuzi ni wanne pekee, jambo ambalo ni kinyume," alisema Mwambigija.

Alisema hata kama akidi ya viongozi hao ingetimia bado jukumu la kuwavua watu nafasi za uongozi sio la kwao kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 7(66) ambayo inaeleza majukumu ya Kamati Tendaji ya Kanda.

Mwambigija alisema yeye anaijua vizuri Katiba ya chama hicho na kwamba amekuwa akifanya kazi vizuri ya kukijenga chama hicho na ndiyo maana wanachama wamekuwa wakimchagua kuwa mwenyekiti kwa muda wa miaka 15 mfululizo.

Vilevile alisema kwa mujibu wa Katiba, vipo vikao ambavyo vinatakiwa kufanyika ili kumvua kiongozi yeyote madaraka lakini yeye pamoja na viongozi wenzake hawajaondolewa kwenye kikao chochote.

Alimtaka Msigwa na wenzake kuacha kufanya kazi kwa mihemuko na badala yake wafuate katiba ya chama ili kuepuka kufanya mambo ambayo yanasababisha taharuki kwa wananchi na wanachama.

Mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Msigwa alitangaza kuwa Kamati Tendaji ya Chama hicho Kanda imewaondoa madarakani viongozi wote 11 wa Kamati Tendaji ya chama hicho Wilaya ya Mbeya Mjini kutokana na utovu wa nidhamu.

Msigwa alisema viongozi hao walionyesha utovu wa nidhamu walipovuruga Mkutano wa Kamati hiyo ya kusuluhisha mgogoro unaoendelea kati ya viongozi hao na wanachama.

Msigwa alisema kutokana na uamuzi huo, viongozi wa chama hicho Mkoa wa Mbeya inatakiwa kuunda kamati maalumu ambayo itakuwa inaendesha shughuli za chama huku akisisitiza kuwa kama viongozi hao watakuwa hawajaridhika wanayo haki ya kukata rufani Kamati Tendaji ya chama hicho Taifa.



Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa (katikati), akiwa na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo pamoja baadhi ya watumishi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), wakiangalia miundombinu ya umeme iliyoharibiwa na watu wasiojulikana hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Maelfu wapata ukombozi wa maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya wakazi 5,000 wa Kata ya Shizuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanatarajiwa kuondokana na kero ya kufuata huduma ya maji umbali mrefu baada ya miezi mradi wa maji wa Inyala- Ilembo utakapokuwa umekamilika.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata hiyo uliokuwa na lengo la kumtambulisha mkandarasi anayetekeleza mradi huo.

Alisema serikali imetoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huku akiwataka wananchi wa kata hiyo kutoa ushirikiano kwa mkandarasi huyo anayetekeleza mradi huo.

"Mradi huu ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha za UVIKO-19, lakini miradi mingine ambayo imetekelezwa kwa mfumo huu ni ya elimu na afya, sasa wananchi mnatakiwa kuhakikisha mnaitunza vizuri," alisema Dk. Chuachua.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema mradi huo utasaidia kuondoa matatizo ya upatikanaji wa maji kwa wananchi wa kata hiyo na kwamba miradi hiyo inamsaidia kupunguza usumbufu kwake.

Alisema Jimbo la Mbeya Vijijini ni kubwa na ramani yake imekaa vibaya hali ambayo huwa inamfanya awe na wakati mgumu kwenye kuwahudumia wananchi.

Alisema yeye ataendelea kufuatilia mara kwa mara mradi huo ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na wananchi waanze kunufaika kama ilivyo lengo la serikali.

Nao baadhi ya wananchi wa kata hiyo, walisema wamekuwa wakifuata huduma hiyo maeneo ya mbali kwenye mito na kwamba mradi huo utasaidia kuwaondolea tatizo hilo.

# Ujenzi barabara kuunganisha bandari waanza

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI imeanza mchakato wa ujenzi wa barabara ya Kajujumele inayounganisha bandari za Itungi na Kiwira kwa kiwango cha lami ili kurahisisha usafiri wa kuingia na kutoka kwenye bandari hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa usafirishaji katika Ziwa Nyasa.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa safari za meli ya Mbeya II ambayo iliharibika baada ya kupigwa na dhoruba ziwani na matengenezo yake yamekamilika, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema barabara hiyo itaanza kujengwa wakati wowote kuanzia sasa.

Alisema kwa sasa serikali imetangaza tenda ya ujenzi wa barabara hiyo na kwamba mkandarasi atakapopatikana ujenzi wake utaanza mara moja.

"Sasa hivi tumetangaza tenda ya ujenzi wa barabara hii, tunachosubiri ni mchakato wa kumpata mkandarasi na punde atakapopatikana kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami itaanza," alisema Homera.

Alisema serikali imeamua kujenga barabara hiyo ili kurahisisha usafiri wa abiria na mizigo kupitia bandari za Kiwira na Itungi ambazo serikali imetumia fedha nyingi kuzikarabati na sasa zipo katika hali nzuri.

Homera alisema kuwa barabara hiyo pia itasaidia meli mpya mbili za mizigo na moja ya abiria ambazo zimejengwa na serikali ndani ya Ziwa Nyasa zifanye kazi kwa ufanisi na kuinua uchumi kwa wananchi wa mwambao wa Ziwa Nyasa na taifa kwa ujumla.

Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abdallah Mohamed, alisema meli ya abiria ya Mbeya II ilikatisha safari zake ndani ya Ziwa Nyasa miezi tisa iliyopita baada ya kupigwa na dhoruba ikiwa katika bandari ndogo ya Matema na kupata hitilafu.

Alisema matengenezo ya meli hiyo yamekamilika na imekaguliwa na Wakala wa Usafiri wa Meli nchini (TASAC) ambao wametoa cheti ya kuiruhusu iendelee na safari zake ndani ya Ziwa Nyasa.

"Januari 27, mwaka huu TASAC walitoa cheti cha ukaguzi wa meli ya MV Mbeya II na kutoa idhini ya meli yetu kuanza tena safari zake ndani ya Ziwa Nyasa, hatua hii itasaidia wananchi kuendelea kupata huduma ya usafiri waliyoikosa kwa zaidi ya miezi tisa," alisema Mohamed.

Baadhi ya wananchi walisema hatua ya meli hiyo kurejesha huduma zake itawasaidia kuondoka na adha ya kukosa usafiri wa uhakika ndani ya Ziwa Nyasa.

"Juliana Mwakyolile alisema baada ya meli hiyo kusitisha safari zake walikuwa wakihatarisha maisha yao kwa kupanda majahazi ambayo hayakuwa na uwezo mzuri wa kuhimili mawimbi ziwani.

"Tulikuwa tunapanda majahazi na mitumbwi na kwa vile mitumbwi hiyo ni midogo tulikuwa tunajazana humo kiasi kwamba tulikuwa tunahatarisha maisha yetu, sasa tunaishukuru serikali kwa kuikarabati meli hii ambayo inatufanya tuwe na uhakika wa kupata usafiri salama," alisema Mwakyolile.

Meli ya MV. Mbeya II ilisitisha safari zake ndani ya Ziwa Nyasa Mwezi, Mei mwaka huu, baada ya kupigwa dhoruba wakati ikitaka kutia nanga kwenye Bandari ya Matema Beach hali iliyosababisha ipate hitilafu na kulazimu ifanyiwe matengenezo.



# ZIPA yatamba kumaliza vikwazo vya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, amesema ofisi yake imejipanga kuhakikisha wawekezaji wanaofika Zanzibar, wanawekeza bila usumbufu wowote.

Alisema hayo jana wakati wa mkutano wa pamoja kati ya taasisi za serikali na ujumbe kutoka Falme za Kiarabu kuhusu masuala ya uwekezaji uliofanyika ofisi za mamlaka hiyo.

Alisema licha ya kuwa wametoa nafasi kwa taasisi kama za uvuvi, afya na utalii na ZIPA inafanya ushawishi mkubwa ili kuona ifikapo mwezi Juni mwaka huu, mambo yawe yamekwishaanza ili kuleta tija kwa Zanzibar na wawakezaji.

Mkurugenzi huyo alisema wakati umefika kwa taasisi hizo kuwa tayari na kuchangamkia tenda bila ya kuchelewa, kufanya mawasiliano na wahusika hao ili mipango yao inakwenda vizuri kama azma ya Rais ya kuhimiza uwekezaji inavyotaka.

Alisema miradi ambayo Falme za Kiarabu imeonyesha nia ya kuwekeza Zanzibar itakuwa na faida kubwa kwa pato la taifa.

Mkurugenzi wa International Holding Company kutoka Falme za Kiarabu, Ali Rashed Al Rashdi, alisema wamefika Zanzibar kujionea fursa ya kuwekeza katika mambo muhimu ikiwamo sekta za utalii, uvuvi na afya ambapo ameridhika na mandhari ya Zanzibar.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Bluu Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema wako tayari kuona uwekezaji huo kwa upande wao unakwenda kwa wakati pasi na tatizo lolote.

Alisema kuwa baada ya kikao hicho, wizara yake itakaa kuona yale yote ambayo wawekezaji hao watakuwa tayari kutaka kuwekeza.

"Wizara ya Uchumi wa Bluu na Maendeleo ya Uvuvi imejipanga katika kuwathamini wawekezaji kwa sababu wanaamini kuwa Zanzibar kuna fursa nzuri kwa wawekezaji hasa katika masuala ya uchumi wa bluu na uvuvi na Zanzibar ina bahari nzuri," alisema.

**Alisema hayo jana wakati wa mkutano wa pamoja kati ya taasisi za serikali na ujumbe kutoka Falme za Kiarabu kuhusu masuala ya uwekezaji uliofanyika ofisi za mamlaka hiyo.**

# Waziri apata jawabu la utatuzi shida ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema wadau wa sekta ya elimu wana wajibu wa kuhakikisha elimu inayotolewa ina ubora wa hali ya juu na inakidhi mahitaji ya Zanzibar na ina viwango vinavyokubalika kimataifa.

Aliyasema hayo jana alipozungumza katika mahafali ya tatu ya Chuo cha Microtech Institute of Business Technology yaliyofanyika viwanja vya Kisonge mjini Zanzibar.

Alisema utamaduni wa ujasiriamali lazima upewe nafasi katika mchakato mzima wa elimu ili kuwawezesha wanafunzi wanapomaliza masomo wawe na uwezo wa kujiajiri.

"Ninyi nyote mnafahamu kuwa nafasi za kazi ni chache na hii siyo kwa Zanzibar peke yake ila ni kwa dunia nzima," alisema.

Alikipongeza chuo hicho kufundisha ujasiriamali na kusisitiza uongozi huo elimu hiyo iwe endelevu ili kukuza ajira kwa kujiajiri na kuajiri vijana wengine.

Alisema kuwa maendeleo ya Zanzibar yanapatikana kwa nguvu kazi yenye ujuzi na uzoefu, hivyo vyuo kama hivyo vina umuhimu katika gurudumu la maendeleo.

Waziri huyo alisema sekta zote za kiuchumi na kijamii zinahitaji watendaji wenye taaluma ili kukuza fani na tija ya uzalishaji mali na utoaji wa huduma.

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi wezake, Farhia Muhamed Ali, alisema wanakabiliwa na kikwazo cha ukosefu wa mitaji wanapotaka kujiajiri wanapomaliza masomo yao.

Alisema jambo hilo linapelekea wahitimu kubaki majumbani wakati wana ndoto na ujuzi wa kujiendeleza kimaisha.

Wanafunzi 243 wamehitimu mafunzo yao chuoni huko kwa fani mbalimbali ikiwamo ya teknolojia ya habari na mawasiliano.




Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai Zanzibar, Zuberi Chembela, akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za makao makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar jana, kuhusu matukio mbalimbali ya kihalifu. PICHA: RAHMA SULEIMAN

# Mbaroni tuhuma dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya.

Watuhumiwa hao walikamatwa kwa nyakati tofauti katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai Zanzibar, Zuberi Chembela, aliwataja watuhumiwa hao ni Sabaha Mbaraka Mabrouk (39), mkazi wa Makorora mkoani Tanga anayedaiwa kukamatwa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar akielekea India.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Januari 27 majira ya saa mbili usiku akidaiwa kuwa na 'unga' aina ya Heroine wenye ujazo wa kilogram 1.6 alioweka katika begi lake.

Alimtaja mtuhumiwa mwingine ni Rehema Mwinyimkuu Mohd (52), mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, aliyekamatwa Januari 31, mwaka huu, majira ya saa nane mchana katika uwanja huo akitokea Afrika Kusini.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na dawa aina ya Heroine zenye ujazo wa kilogramu 4.36 akidaiwa kuzificha katika begi lake.

Alieleza kuwa watuhumiwa wote hao wapo chini ya ulinzi, uchunguzi na upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi Zanzibar linaendelea kupambana na vitendo vya uhalifu ikiwamo dawa za kulevya ambapo matukio 686 yameripotiwa mwaka 2021 kulinganishwa na matukio 587 yaliyoripotiwa mwaka 2020.

Chembela alisema kuwa katika mapambano ya dawa za kulevya, yanakabiliwa na tatizo la muhali kwa kuwa watuhumiwa wa makosa hayo wanajulikana katika jamii, lakini imekuwa ni shida kupata ushirikiano katika ushahidi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO!!
### AFRIWELD INDUSTRIES LTD
### Nafasi ya kazi

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35

**Nafasi:** Mauzo

MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!! wahi sasa Kupata nafasi nzuri!! Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**

Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni

**01/01/2022 MPAKA 15/02/2022**

**Asante**

116653602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NO.293 YA 2021**

**YAPI MARKEZI INSAAT VESANY ANONISM SIRKET……………………MDAI**
**VERSUS**
**NYANZO AFRICA………………………………..MDAIWA**
**KWA:**
**NYANZO AFRICA**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii ya wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 02 mwezi 02 mwaka 2022 saa mbili (2:30) kamili asubuhi.

Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetoilewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 19 mwezi January 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NO.292 YA 2021**
**YAPI MARKEZI INSAAT VESANY ANONISM SIRKET……………………MDAI**

**VERSUS**

**MAPPLE RESOURCES LTD……………………..MDAIWA**
**KWA:**
**MAPPLE RESOURCE LTD**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii ya wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 02 mwezi 02 mwaka 2022 saa mbili (2:30) kamili asubuhi.

Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetoilewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 19 mwezi January 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI

---

## TANGAZO LA KUPOTEA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

Pearl Lucas Musiba anatangaza kupotelewa na umiliki wa kiwanja namba 162 Kitalu "T" kilichopo Majengo Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo Karibu au awasiliane na Pearl Lucas Musiba kwa simu namba 0765944930.

**Rb namba SHI/SHI/RB/46467/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**JUSTINA LIANA MALISA………MAREHEMU**
**ROSE BERNARD MASHINGA……MUOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 10 mwezi wa februari,mwaka 2022

Imewasilishwa mwanga leo tarehe 27 mwezi wa januari,mwaka 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

---

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, CAP 117 RE 2019**
**DEEP POLL**



BY THIS DEED, I WILIBATI PETRO MKUDE of KILUVYA MADUKANI- PWANI, Tanzania, do hereby wholly absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former name of WILIBERD PETER MKUDE and adopt as from the date of this Poll and in substitution of my former name, the name WILIBATI PETRO MKUDE. For the purposes of evidence of such determination, I hereby declare, that I shall at all times hereinafter in all records, deeds, documents and other writings and in all actions, suits and proceedings as well in all public and private dealings the transactions and occasion whatsoever use and subscribe the said name of WILIBATI PETRO MKUDE as my name in lieu of and substitution for my former name WILIBERD PETER MKUDE.

AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whosoever at all times after date hereon to designate, describe and address me by the adopted name of WILIBATI PETRO MKUDE.

IN WITNESS WHEREOF, I hereon substitute my old name of WILIBERD PETER MKUDE.

By the new name of WILIBATI PETRO MKUDE.

SWORN and SIGNED at Dar es Salaam by
The said WILIBATI PETRO MKUDE
This 20 day of October 2021

BEFORE ME:
NAME:
SIGNATURE:
ADDRESS:
QUALIFICATION:

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY)**
**(ONE STOP JUDICAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**
**In the matter of the estate of the late**
**Paul Frederick Gatrell………………Deceased**
**And**
**In the matter of an application for sealing of the letters of administration**
**By**
**Helen De Vere Van Der Linden…………1st Application**
**Clare Lina Pitman………………………2nd Application**
**NOTICE OF APPLICATION FOR RESEALING**
**(Rule 99)**

Notice is hereby given that an application has been made to this Court for sealing of the letters of administration of the estate of Paul Frederick Gatrell, late of Malawi, who died at Blantyre Adventist Hospital in Malawi on the 15th day of September 2017, granted to Helen De Vere Van Der Linden and Claire Lina Pitman, of Malawi by the High Court of Malawi and that the said application will be heard at this Court by a Judge in Chambers on the **14th day of February, 2022 at 9:00 O'clock in the morning.**

**Dated at Dar es salaam, this 1st day of December, 2021.**

HIGH COURT OF TANZANIA

Deputy Registrar

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**CYPRIAN JOSEPH KADOPE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **HORSE** yenye namba za usajili **T 431 ATE** na kadi ya gari aina ya **TRAILER** yenye namba za usajili **T 720 DGF**,yeyote atakayeziokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **MKB/RB/358/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

COLLIN JAMES HIGGINS Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya GARI (Mitsubishi Fuso) yenye namba za usajili T 820 AQR,Chasis namba FK618K523625 na Engine namba 6D17868479 yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba 0655753075 MOR/MOR/RB/44575/2022

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU GEOFREY STEPHEN KONZO anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina la MRIMI INTERNATIONAL TANZANIA na namba za usajili T770DCU aina ya CANTER MITSUBISH Rangi ya njano yenye Chasis No. TYAFB634B4DS00843 Engine No. Z606FN.

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba DOD/DOD/RB/40208/2022

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**FATIMA ALLY LILANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3432/0004 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya NJENGWA mwaka 2017,

Yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa MTW/MTW/RB/551296/2020

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU SULEMAN NASSOR SULTAN anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Tractor, yenye namba za usajili T 204 AMF. Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye. Taarifa ya polisi: MUR/BUN/RB/37489/2022

---

## KUPOTEA KWA HATI YANYUMBA(MTUMBA

JOSEPH RENATUS SENGASENGA Anatangaza kupotelewa kwa Hati ya nyumba(mtumbe) BLOCK NO:AR 103 MTUMBA yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba 0715819940 MOR /MOR/RB/10981/2022

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watu 10 mbaroni tuhuma za mauaji

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu 10 akiwamo mganga wa kienyeji kwa tuhuma za mauaji ya dereva teksi na mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, alisema jana kuwa katika tukio la kwanza, jeshi hilo linawashikilia watu wanne akiwamo mganga wa kienyeji kwa tuhuma za mauaji ya Respicius Anastaz (55) dereva teksi.

Alisema tukio hilo lilitokea Januari 26, mwaka huu, majira ya saa 4 :15 usiku katika kijiji cha Kasungamile wilayani Sengerema.

Kamanda Ng'anzi alisema katika tukio hilo, dereva teksi huyo alikodiwa na watuhumiwa ambao ni Sylivester Renatus (30 ) na mke wake, Elizabeth Jackson (23) kutoka Buzuruga Mwanza kwenda Sengerema.

"Walipofika maeneo ya kijiji cha Kasungamile walifanya unyama huo na baada ya kufanya mauaji hayo walikwenda kwa mganga wa kienyeji ili wasafishwe na dawa wasikamatwe na polisi," alisema.

Alisema ilipofika majira ya saa 4:00 usiku, polisi wakiwa katika doria walikuta gari hilo likiwa limetelekezwa katikati ya barabara ndipo ufuatiliaji wa haraka ulifanyika na kuwakamata watuhumiwa pamoja na mganga wa kienyeji, Ryabakamba Sekelwa (30) na mume wake, Robert Daud (42)," alieleza Kamanda.

Alieleza kuwa kiini cha tukio hilo kinasadikiwa ni kutaka kujipatia gari hilo lenye namba T620 CGN.

Kuhusu tukio la mwanafunzi wa SAUT, Nicholus Telesphory (25) alisema aliuawa na kundi la wahalifu kwa kupigwa mawe na fimbo sehemu mbalimbali za mwili wake kwa tuhuma za wizi wa televisheni.

Alisema Telesphory alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Mkoa Sekou - Toure.

# Jaji aanika kikwazo kesi za udhalilishaji

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

JAJI Mkazi Kisiwani Pemba, Ibrahim Mzee Ibrahim, amesema changamoto kubwa inazo zikabili Mahakama za Pemba wakati wa kusikiliza kesi za udhalilishaji wanawake na watoto ni jinsi ya mashahidi wanavyobadilika.

Jaji Mzee amesema mashahidi hao wanabadilika wanapokwenda kuchukuliwa maelezo Polisi na wanapokwenda mahakamani kutoa ushahidi wanatofautiana.

Akijibu swali la waandishi wa habari waliotaka kujua kikwazo kikubwa kinachoikumba mahakama kisiwani Pemba wakati wa kusikiliza kesi hizo, Jaji Mzee alisema kuna baadhi ya watuhumiwa wa ubakaji wakishabaka huenda na nasaha kumuoa mtoto wa kike anapokwenda mahakamani kutoa ushahidi.

Alisema kutokana na hali hiyo mwanamke anakataa anasema aliyepo mbele yake ni mume wake, hivyo hayuko tayari kumtolea ushahidi.

Alisema wakati mwingine aliebakwa akienda mahakamani hudai kuwa mtuhumiwa aliyepo mbele yake ndo mara yake ya kwanza kumuona na kudai kuwa wazee wake baba au mama tu ndio walio taka asema kabakwa.

Jaji alisema hali hiyo inaifanya mahakama kukosa ushahidi wa wazi kumtia mtuhumiwa hatiani na kumpa adhabu stahiki kwa mujibu wa sheria.

Alisema inapotokea hali hiyo mahakama haina la kufanya kwa kuwa sheria haimlazimishi mwanamke kumtolea mumewe ushahidi, hivyo kufanya baadhi ya kesi kuharibika na baadhi ya watu wasio na uelewa kuilalamikia mahakama.

Alikuwa akizungumzia maadhimisho ya Siku ya Sheria inayotarajiwa kufikia kilele chake Februari 07, mwaka huu, na kwamba kutokana na kukithiri kwa vitendo vya udhalilishaji, wamedhamiria kutoka na kwenda kwa wananchi kutoa elimu juu ya hali hiyo.

"Tumeandaa outreach Program kutoka kwenda mikoa yote miwili kukaa na wadau kuwapatia elimu kwa lengo la kuweka sawa kasoro zinazojitokeza katika kuripoti vitendo hivyo, ukiwa ni mchango wetu (mahakama) katika mapambano dhidi ya matendo hayo mabaya yaliyoikumba nchi yetu," alisema Jaji Mzee.

Aidha Jaji huyo alisema katika shamra za madhimisho ya Siku ya Sheria pia wamekusudia kuwa na kongamano kuhusu vita dhidi ya mapambano ya dawa za kulevya hasa kwa upande wa kisiwani Pemba kwa lengo la kupendekeza nini kifanyike kudhibiti uingizwaji wa dawa hizo kisiwani humo.



Meneja mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), Zilipa Mgeni (kushoto), akitoa maelekezo ya mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wa wanaotoka mazingira magumu ambao ni wanufaika wa mradi huo, unaowasaidia elimu ya ujasiriamali na mtaji kwa vijana 770 kutoka Kata tatu za Ihanu, Mdabulo na Luhunga, Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Daraja la Tanzanite lilivyowakuna wengi Dar

**Na Jenifer Gilla**

DARAJA la Tanzanite lililojengwa juu ya bahari kutoka eneo la Aga Khan mpaka Oysterbay lilianza kutumika jana, huku baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam wakimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kukamilika kwake.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alitangaza kikamilika kwa ujenzi huo alipofanya ziara ya kulikagua Jumapili.

Jana asubuhi magari pamoja na watu binafsi walionekana wakipita katika daraja hilo, baadhi yao walionyesha kufurahia ujenzi wa daraja hilo na kummwagia sifa Rais Samia.

Zulekha Brown, mkazi wa Tegeta, jijini Dar es Salaam, aliyepita asubuhi jana akitokea kuekelea katikati ya Jiji, alisema daraja hilo litapunguza foleni iliyosumbua kwa muda mrefu katika eneo hilo.

"Nimefurahi sana kukamilika kwa daraja hili kwa kuwa naamini litapunguza msongamano wa magari uliokuwa katika makutano ya daraja la Salender ambao ulikuwa unasababisha tunachelewa kazini," alisema Zulekha.

Zulekha alisema alikuwa anatumia takribani nusu saa kuvuka kipande cha daraja Salender nyakati za asubuhi na jioni, lakini sasa foleni hiyo itapungua kwa kuwa wale wanaokwenda Oysterbay watalazimika kutumia daraja hilo. Ernest Shayo, mkazi wa Mbezi, alisema daraja hilo litamsaidia kufika kazini kwa wakati kwa kuwa limeelekezwa ofisi yake iliko.

"Mimi nafanyakazi maeneo ya Aga Khan Hospitali, kwa hiyo njia hii ni karibu na ofisini kwangu, kwa kweli nafurahi kuona kuwa sitolazimika kuamka saa kumi na moja alfajiri ili kufidia ile foleni mataa ya Salender, naishukuri sana serikali ya Mama Samia,"alisema Ernest.

Msemaji wa Klabu ya Yanga, Haji Manara, aliyepita kwenye daraja hilo, alieleza kufurahishwa na ujenzi huo.

"Katika mazoezi yangu ya leo nimefika hadi Tanzanite Bridge, nimpongeze Rais Samia kwa ujenzi wa daraja hili zuri la kisasa lenye viwango vya kimataifa," aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Naye Burton Mwemba alisema ujenzi huo umeifanya Dar es Salaam kuwa na mwonekano wa kimataifa na kuiongezea hadhi Tanzania.

"Kuna vitu tulikuwa tunaviona kupitia kwenye TV (runinga) au kwenye movie (sinema) tu, daraja hili nilikuwa naliona huko na kwenye vitabu, lakini leo naliona Dar es Salaam, ahsante sana Rais Samia,"aliandika Burton.

Daraja hilo lenye urefu wa KM 1.03 na upana wa mita 20.5, limegharimu zaidi ya Sh. bilioni 240, likijengwa na mkandarasi GS Engineering and construction.

# NYOTA 10 CRDB BANK TAIFA CUP 2021 WAPEWA UFADHILI MASOMO

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetangaza ufadhili wa masomo wa Sh. milioni 10 kwa wachezaji 10 bora wa mashindano ya Taifa ya mpira wa Kikapu "CRDB Bank Taifa Cup" 2021.

Akizungumza katika hafla ya kutangaza ufadhili huo jana, ambayo pia ilionyeshwa mubashara kupitia chaneli ya michezo ya Azam TV, Meneja Mwandamizi wa Uwekezaji katika Jamii Benki ya CRDB, Joycelean Makule, alisema ufadhili huo wa masomo kwa wachezaji ni mwendelezo wa jitihada za benki hiyo katika kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupitia michezo.

Joycelean alisema benki hiyo kupitia sera yake ya Uwezeshaji katika Jamii (CSI Policy), imekuwa ikiwekeza katika michezo ya vijana kwa kuamini kuwa inasaidia kuongeza ushiriki wao katika shughuli mbalimbali ikiwamo elimu ili kusaidia kuwajenga kwa ajili ya maisha ya baadaye.

"Katika CRDB Bank Taifa Cup, wapo vijana wengi ambao bado wapo masomoni katika ngazi mbalimbali. Hivyo benki iliona ni vema kuambatanisha suala la elimu na michezo kwa kutoa ufadhili wa masomo kwa vijana ambao wameonyesha uwezo mkubwa kwenye mashindano ya CRDB Bank Taifa Cup," alisema Joycelean.

Akizungumzia kuhusu msukumo uliosababisha benki hiyo kudhamini masomo ya wachezaji wa mpira wa kikapu, Joycelean alisema mchezo huo umekuwa haupewi sana kipaumbele kulinganisha na michezo mingine, hivyo kuwakatisha tamaa vijana wengi ambao wamekuwa wakionyesha vipaji.

"Baada ya mchakato mrefu wa kufanya tathmini ya uwezo ulioonyeshwa na vijana pamoja na kufuatilia taarifa zao za kielimu kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), tumefanikiwa kukamilisha zoezi hilo na leo (jana) tupo hapa kwa ajili ya kutangaza vijana waliofanikiwa kupata nafasi hizo za ufadhili wa masomo kwa mwaka 2021/2022," alisema Joycelean.

Huu ni mwaka wa pili kwa Benki ya CRDB kutoa ufadhili wa masomo kwa wachezaji bora wa mchezo wa mpira wa kikapu kupitia CRDB Bank Taifa Cup. Mwaka jana benki hiyo ilitoa ufadhili wa masomo wa jumla ya Sh. milioni 50 kwa vijana 25.

"Tunajivunia kuendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa vijana kupitia mchezo huu kwani tunaamini utasaidia kufikia ndoto zao kupitia elimu," aliongezea Joycelean.

Akizungumza kwa niaba ya vijana waliopata ufadhili wa masomo, mchezaji wa timu ya wanawake ya mpira wa kikapu Mkoa wa Kilimanjaro, Jesca Mbowe, ambaye anasoma Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Shahada ya Usimamizi wa Utalii, ameishukuru Benki ya CRDB kwa ufadhili huo, huku akieleza kwamba utakuwa chachu kwao kusoma kwa bidii ili kufikia malengo yao.

Kwa upande wa Makamu wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania, Rwehabura Balongo, ameishukuru Benki ya CRDB kwa kuendelea kuwekeza katika mpira wa kikapu huku akisema udhamini huo wa masomo utakwenda kuleta hamasa zaidi kwa vijana wengi kushiriki katika mchezo huo.

Balongo aliishukuru pia Benki ya CRDB kwa kuendelea kuwa mdhamini wa mashindano ya Taifa ya mpira wa Kikapu, ambapo tangu benki hiyo ianze kushirikiana na TBF kumekuwa na mwamko mkubwa katika mchezo huo.

Benki ya CRDB mwaka jana iliongeza udhamini kwenye Taifa Cup hadi kufikia Sh. milioni 300 ambapo timu 32 za mpira wa kikapu kwa upande wa wanaume na wanawake zilichuana vikali.

Timu za wanawake na wanaume za mpira wa kikapu Mkoa wa Dar es Salaam ziliibuka kidedea katika mashindano hayo yaliyofanyika viwanja vya Chinangali, Dodoma.



Mchezaji wa timu ya mpira wa kikapu wa timu ya Unguja, Karen Erling Andersen (katikati), akizungumza wakati wa kutangaza ufadhili wa masomo wa Sh. milioni 10 kwa wachezaji 10 bora wa mashindano ya Taifa ya mpira wa Kikapu "CRDB Bank Taifa Cup" 2021, katika kipindi cha michezo kichoonyeshwa mubashara kupitia chaneli ya michezo ya AzamTV, jijini Dar es salaam jana. Wengine pichani kutoka kulia ni Jesca Mbowe (timu ya Kilimanjaro), Judith Kovaga (timu ya Iringa), Maria Alex (timu ya Tanga) pamoja na Subira Komba (timu ya Iringa). **MPIGAPICHA WETU**

# *TAFF yasaka kocha Tembo Warriors*

**Na Saada Akida**

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu nchini (TAFF), Peter Sarungi, amesema wako katika mchakato wa kutafuta kocha kwa ajili ya kuimarisha timu ya Taifa, 'Tembo Warriors' kuelekea katika mashindano ya Kombe la Dunia.

Tembo Warriors wataiwakilisha nchi katika mashindano hayo kwa mara ya kwanza ikiwa ni miongoni mwa mataifa manne ya Afrika yanayotarajiwa kushiriki michuano hiyo itakayoanza Oktoba 1-9, mwaka huu jijini Istanbul, Uturuki.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Rais wa TAFF, Sarungi alisema mchakato huo unaendelea na tayari wameanza mazungumzo na baadhi ya makocha kutoka nje kwa lengo la kuimarisha benchi lao la ufundi.

Alisema makocha ambao wanazungumza nao ni Stephen Richard na Nana Kwame ambaye alikuwa kocha wa timu ya Ghana ambao ni mabingwa wa CANAF.

"Kwame pia ni kocha wa klabu ya Konye inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka la wenye Ulemavu nchini Uturuki, kocha mwingine ambaye yuko kwenye mazungumzo ni Willis Odhiambo Otieno wa timu ya Taifa ya Kenya," alisema Sarungi na kuongeza.

"TAFF imedhamiria kufanya vema kwenye mashindano ya Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania na soka la wenye ulemavu," alisema Sarungi. Alisema Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu Duniani (WAFF), limetangaza tarehe ya kuanza mashindano hayo na mji yatakapofanyika, hivyo sasa wao wanaangalia lini timu iingie kambini.

"Tunashukuru tarehe ya mashindano imetoka na TAFF na serikali tumeanza maandalizi ya timu yetu, kwa sasa yamebaki mambo machache ili timu iingie kambini kuanzia mwezi ujao," alisema Sarungi.

## Mbio kupanda Ligi Kuu Z'bar zapamba moto

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MBIO za kusaka nafasi ya kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao, zimeendelea kushika kasi kwenye Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inayoendelea kwa sasa.

Ligi hiyo inajumla ya timu 16 ambapo timu mbili zitapanda daraja kwa kanda husika wakati nne zikishuka daraja na kurudi kushiriki ligi za mikoa.

Katika mwendelezo wa ligi hiyo ambayo imeendelea katika viwanja viwili juzi, kwenye Uwanja wa Mau A timu ya Ngome iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Bridge Star huku katika dimba la Mchangani, Mchangani FC ikitoshana nguvu na Jang'ombe Boys kwa kutoka na sare ya bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kocha wa Ngome FC, Suleiman Mohmed "Mo", alisema malengo yake makubwa ni kuhakikisha timu hiyo inapanda daraja msimu huu.

Alisema katika usajili wa dirisha dogo, amesajili vizuri baada ya kuangalia mapungufu waliyonayo, hivyo kupitia mchezo huo waliopata ushindi unazidisha matumaini kwao ya kupanda daraja.

"Hamu yetu msimu huu ni kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu msimu ujao, ndio maana katika dirisha dogo tumefanya usajili kulingana na mapungufu yaliyokuwapo katika dirisha kubwa," alisema.

Kwa upande wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum, alisema katika Ligi Daraja la Kwanza kuna changamoto ndogo ndogo ambazo zinajitokeza ikilinganishwa na awali msimu ulipoanza.

Alisema awali klabu zilikuwa na changamoto nyingi ambazo zilitokana na mazoea, kubwa ikiwa kutumia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao ambapo changamoto hiyo imepungua kwa kiasi kikubwa baada ya kupewa elimu ya matumizi ya mfumo huo.

"Kwa kipindi kifupi msimu huu, tumeweza kupunguza changamoto nyingi mno kwa hizi klabu za daraja la kwanza ikiwamo kufika uwanjani kwa muda sahihi," alisema.

Aidha, alisema Bodi ya Ligi Zanzibar itaendelea kutoa elimu mara kwa mara kwa klabu za kanda kuhusu masuala mazima ya kusoma na kufuata kanuni ya mashindano ili kupunguza migogoro hasa kipindi cha usajili wa wachezaji kinapowadia.

**Akizungumza na gazeti hili juzi, Kocha wa Ngome FC, Suleiman Mohmed "Mo", alisema malengo yake makubwa ni kuhakikisha timu hiyo inapanda daraja msimu huu.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE SAFI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, amekubali kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho wa bila malipo wakati mkataba wake na Paris St-Germain utakapomalizika msimu wa majira ya joto. (**Bild**)

### LACAZETTE ASUBIRIWA LYON

KLABU ya Lyon ilijaribu kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Ufaransa, Alexandre Lacazette wakati wa uhamisho wa wachezaji, klabu hiyo ya Ligue 1 sasa italazimika kufikia makubaliano na mshambuliaji wao huyo wa zamani mwenye umri wa miaka 30 msimu wa majira ya joto. (**L'Equipe**)

### RAMSEY ATUA RANGERS

KIUNGO wa kati wa Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 31, alikuwa anawaniwa na Brentford, West Ham, Aston Villa, Crystal Palace, Wolves na Arsenal kabla ya kujiunga na Rangers kutoka Juventus. (**JOE**)

### BISSOUMA NUSURU ATUE VILLA

KLABU ya Aston Villa ilifikiria kumnunua kwa kima cha pauni milioni 50 mchezaji wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25. (**Mail, via Birmingham Ma**il)

### UNITED YAMZUIA HENDERSON

MANCHESTER United ilizuia uhamisho wa mkopo kutoka kwa golikipa wao, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 24 kwenda Watford. (Manchester Evening News)

### CHELSEA YAGONGA MWAMBA

OMBI la Chelsea la kutaka kumnunua mshambuliaji wa Charlton mwenye umri wa miaka 18, Mason Burstow lilikataliwa mara mbili. (**Talksport - via Sun**)

### ANCELOTTI KUFANYA MTIHANI

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, ameambiwa lazima afanye upya mtihani wa Uefa wa ukocha baada ya muda wa cheti chake kumalizika. (**Corriere dello Sport - via Talksport**)

### GUEYE ARUDI EVERTON

KLABU ya Everton imefanikiwa kumnunua mchezaji wao wa zamani na kiungo wa kati wa Senegal, Idrissa Gueye mwenye umri wa miaka 32, kutoka Paris St-Germain dakika za mwisho kabla ya dirisha la uhamisho la Januari kufungwa. (**Athletic - via Express**)

### BARCA YAMGOMEA DEMBELE

BARCELONA ilitathmini uwezekano wa kumpelekea mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24 kwenda Arsenal kwa mkopo kama sehemu ya makubaliano ya kumleta mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye miaka 32. (**Independent**)

### LINGARD AWEKEWA NGUMU

JESSE Lingard wa Manchester United mwenye umri wa miaka 29, aliambiwa kuwa hawezi kuondoka katika klabu hiyo siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili. (**Manchester Evening News**)

### SABABU LUIZ KUGOMEWA VILLA

ASTON Villa pia ilikataa ofa tatu za kumuuza kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz Januari, kwa matumaini kwamba kiungo huyo mwenye umri wa miaka wa 23, atakubali kusaini mkataba wa muda mrefu. (**Athletic**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# AUBAMEYANG RASMI SASA MALI YA BARCA

●●● Alitarajiwa kuondoka kwa mkopo, lakini amesajiliwa kwa mkataba wa kudumu na amepunguziwa mshahara wake wa pauni...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wamekamilisha usajili siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili la Januari kwa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, hajawachezea 'Washikabunduki' hao tangu Desemba mwaka jana baada ya kuvunja sheria za kinidhamu na akapokonywa unahodha.

Na miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, walikamilisha dili hili na kuwazidi Juventus wakimtwaa mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon.

Aubameyang alitarajiwa kuondoka kwa mkopo, lakini Barca wamemsajili kwa mkataba wa kudumu na amekubali kupunguziwa mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki aliokuwa akichukua kule Arsenal.

Dili hili lilithibitishwa rasmi jana Jumanne na klabu hizo mbili baada ya usajili huo ambao haukutarajiwa na wengi.

Arsenal inatarajia kuokoa bili ya mshahara wa pauni milioni 25 na fedha hizo zitatumika katika kuimarisha kikosi chao kipindi cha majira ya joto kijacho.

Aubameyang, ambaye amefunga mabao 68 katika mechi 128 za Ligi Kuu England kwa klabu hiyo ya London Kaskasini, anatarajia kurudi kwenye kiwango chake cha kufunga mabao kwa klabu yake hiyo kama ilivyokuwa wakati akiwa pale kweye dimba la Emirates.

Amejiunga na Ferran Torres pale Katalunya baada ya nyota huyo wa zamani wa Manchester City kusajiliwa mwanzoni mwa dirisha dogo kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha Xavi.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 896

MECHI KALI
BERKINA FASO
VERSUS
SENEGAL
1 | 4.98
X | 3.04
2 | 1.85

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BIDHAA ZA GREENWOOD ZAONDOLEWA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeondoa bidhaa zote za Mason Greenwood kwenye soko la mtandaoni la klabu hiyo kutokana na madai yanayomwandama mshambuliaji huyo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, alikamatwa kwa tuhuma za ubakaji na unyanyasaji baada ya madai yaliyotolewa na mpenzi wake katika mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na picha na sauti.

Man United imemsimamisha mchezaji huyo wa kimataifa wa England, ambaye hataruhusiwa kufanya mazoezi na timu au kushiriki katika mechi hadi hapo itakapotangazwa vinginevyo.

Polisi wa Manchester walithibitisha kuwa walimkamata Jumapili, huku nyota huyo akiwekwa kizuizini, ambapo alikaa usiku kucha kwa mahojiano.

'Masheteni wekundu' hao sasa wamehakikisha bidhaa za Greenwood zisipatikane kwenye manunuzi katika duka lao la mtandaoni.

Man United itarejea uwanjani kucheza na Middlesbrough katika mchezo wa raundi ya nne ya Kombe la FA Ijumaa jioni, lakini Greenwood hatashiriki katika kikosi hicho cha kocha wa muda, Ralf Rangnick.







# Mbappe, Real Madri[…] wafikia makubaliano[…]

**PARIS,** Ufaransa

NDOTO ya Kylian Mbappe kujiunga na klabu ya Real Madrid sio siri tena, ile shauku yake ya kutaka kucheza kwenye timu hiyo ya nchini Hispania sasa inakwenda kutimia baada ya kuingia makubaliano ya awali, kwa mujibu wa Marca.

Baada ya miezi kadhaa ya tetesi kuhusu Mbappe wapi atakwenda akimaliza mkataba wake na Paris Saint Germain, sasa anajiandaa kuhamia kwenye klabu ya ndoto yake mwishoni mwa msimu huu kama mchezaji huru.

Kupatikana kwake huru hakutamfanya kuwa mchezaji v[…] bei chee la hasha, usajili wa[…] kwenda klabu ya Real Madr[…] utamfanya kuwa mchezaji an[…] elipwa fedha nyingi zaidi kuli[…] mchezaji yeyote.

Awali, kulikuwa na taar[…] kuwa Mbappe alikuwa anafikir[…] kuongeza mkataba na miam[…] hiyo ya Jiji la Paris kwa kusai[…] mkataba wa muda mfupi, laki[…] inaonekana kuwa hilo limet[…] piliwa mbali.

Mbappe alijiunga na PSG mw[…] ka 2017 akitokea klabu ya As M[…] naco kwa usajili wa mkopo kab[…] ya kusajiliwa moja kwa moja [...] klabu hiyo.

,686,220

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/02/22 | 18:00 | Hull City vs Preston | 2.55 | 3.25 | 2.80 |
| 02. 05/02/22 | 18:30 | Maritimo vs GD Estoril | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 05/02/22 | 19:00 | St Etienne vs Montpellier | 2.57 | 3.31 | 2.67 |
| 04. 05/02/22 | 20:30 | Swansea vs Blackburn | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 05. 05/02/22 | 21:00 | Pacos Ferreira vs Portimonense | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 06. 05/02/22 | 23:00 | Twente vs Vitesse Arnhem | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 07. 06/02/22 | 16:00 | Valencia vs Real Sociedad | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 08. 06/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Galatasaray | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 09. 06/02/22 | 16:00 | Amorebieta vs Real Oviedo | 2.79 | 3.04 | 2.55 |
| 10. 06/02/22 | 17:00 | Sampdoria vs Sassuolo | 2.81 | 3.56 | 2.36 |
| 11. 06/02/22 | 18:15 | Barcelona vs Atletico Madrid | 2.40 | 3.26 | 2.97 |
| 12. 06/02/22 | 20:00 | Udinese vs Torino | 2.86 | 3.21 | 2.51 |
| 13. 06/02/22 | 20:30 | Betis vs Villarreal | 2.33 | 3.44 | 2.94 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 02/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2571 | Bangkok Utd vs Pattaya United FC | 1.40 | 4.31 | 6.52 |
| 14:15 | 3091 | PSM Makassar vs Persib Bandung | 4.53 | 3.33 | 1.73 |
| 15:25 | 2152 | AL Jeel vs Al Orubah | 2.80 | 2.90 | 2.51 |
| 15:30 | 4732 | EN Paralimni vs Onisilos Sotira FC | 1.51 | 4.05 | 5.20 |
| 15:30 | 5957 | Ermis Aradippou vs Anagennisi Derynia FC | 1.33 | 4.51 | 8.07 |
| 15:55 | 2708 | AL Akhdood vs Al Qadisiyah | 2.85 | 3.10 | 2.60 |
| 16:00 | 1195 | Zanaco vs Forest Rangers | 2.12 | 2.94 | 3.47 |
| 16:00 | 2848 | O F Ierapetras vs Karaiskakis | 1.65 | 3.48 | 4.83 |
| 16:00 | 3077 | Ergotelis vs Kissamikos | 2.51 | 2.85 | 2.85 |
| 16:00 | 3483 | Pierikos Katerini vs PO Triglias | 3.50 | 2.83 | 2.17 |
| 16:00 | 4150 | AE Larissa vs AO Nea Kavala | 1.43 | 3.76 | 7.52 |
| 16:00 | 4458 | Asteras Tripolis vs PAS Giannina | 1.84 | 3.16 | 4.63 |
| 16:10 | 1651 | AL Ain vs Jeddah Club | 2.41 | 2.94 | 2.89 |
| 16:30 | 1316 | Vibonese Calcio vs Virtus Francavilla | 3.86 | 3.22 | 2.00 |
| 16:30 | 1818 | Catanzaro vs AZ Picerno | 1.54 | 3.90 | 6.60 |
| 16:30 | 2331 | Imolese Calcio vs Viterbo Calcio | 2.29 | 3.05 | 3.35 |
| 16:30 | 2364 | Virtus Entella vs Aquila 1902 Montevarchi | 1.32 | 5.20 | 9.20 |
| 16:30 | 3432 | Olbia Calcio vs US Ancona 1905 | 2.70 | 3.10 | 2.75 |
| 16:30 | 4035 | Paganese vs Latina | 2.32 | 3.10 | 3.30 |
| 16:30 | 5231 | Nuova Monterosi vs Bari | 6.60 | 3.95 | 1.52 |
| 17:00 | 2595 | Paeek vs AEK Larnaca | 6.38 | 3.87 | 1.46 |
| 17:00 | 5356 | East Bengal vs Chennaiyin FC | 2.89 | 3.28 | 2.23 |
| 18:15 | 1572 | AL Kawkab vs Hajer Club | 2.60 | 2.89 | 2.70 |
| 18:15 | 2164 | OFI Crete vs Panathinaikos | 3.45 | 2.96 | 2.24 |
| 18:15 | 4538 | Olympiakos vs Panetolikos | 1.23 | 5.73 | 11.86 |
| 18:15 | 4737 | Psis Semarang vs Persebaya Surabaya | 3.50 | 3.25 | 2.14 |
| 18:15 | 5864 | FK Sumgayit vs Gabala | 2.73 | 3.07 | 2.45 |
| 18:30 | 4281 | Atletico Madrid W vs Madrid Ccf W | 1.24 | 5.57 | 8.83 |
| 19:00 | 2437 | Sevilla FC W vs Villarreal CF W | 1.55 | 4.34 | 4.44 |
| 19:00 | 5781 | Olympiakos Nicosia vs Apoel Nicosia | 3.09 | 2.95 | 2.29 |
| 20:00 | 2718 | CD Roda vs CF Villarreal C | 2.80 | 2.85 | 2.56 |
| 20:00 | 2888 | Rio Ave vs Covilha | 1.58 | 3.71 | 5.47 |
| 20:30 | 1681 | Volos vs Ionikos Nikea FC | 1.79 | 3.29 | 4.72 |
| 20:30 | 4686 | Aris Salonica vs AEK Athens | 2.75 | 2.94 | 2.70 |
| 20:45 | 5096 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 2.82 | 3.51 | 2.30 |
| 21:00 | 2419 | GD Chaves vs Varzim | 1.70 | 3.57 | 4.60 |
| 21:00 | 3184 | Duisburg vs Osnabruck | 3.05 | 3.34 | 2.21 |
| 21:00 | 4426 | Leixoes vs Mafra | 2.68 | 3.07 | 2.59 |
| 21:30 | 5700 | Bangu RJ vs Volta Redonda RJ | 3.22 | 3.27 | 2.07 |
| 22:00 | 1584 | Rayo Vallecano vs Mallorca | 2.02 | 3.26 | 3.66 |
| 22:00 | 3632 | Benfica vs Gil Vicente | 1.29 | 5.34 | 9.10 |
| 22:00 | 3804 | Burkina Faso vs Senegal | 4.98 | 3.04 | 1.85 |
| 22:30 | 4985 | Felgueiras vs SAO Joao Ver | 2.08 | 3.19 | 3.28 |
| 22:30 | 5778 | Apollon Smyrnis vs PAOK | 6.93 | 3.96 | 1.47 |
| 22:45 | 2872 | Celtic vs Rangers | 2.16 | 3.30 | 3.25 |
| 22:45 | 5736 | Huddersfield vs Derby | 2.00 | 3.24 | 3.68 |
| 22:45 | 5880 | KAA Gent vs Brugge | 2.54 | 3.37 | 2.54 |
| 23:00 | 4897 | Anadia FC vs Lusitania | 2.60 | 3.17 | 2.50 |
| 23:00 | 5366 | Valencia vs Cadiz CF | 1.66 | 3.74 | 4.83 |
| 23:45 | 3986 | Belenenses vs Sporting Lisbon | 11.78 | 5.70 | 1.23 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# AZAM SASA KAMILI, DUBE, KANGWA WATUA

Na Adam Fungamwango

WACHEZAJI watatu wa Azam waliokwenda kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) nchini Cameroon, wakiwa na timu ya Taifa ya Zimbabwe, wamewasili nchini tayari kwa kuitumikia klabu hiyo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', amesema kuwa wachezaji hao waliwasili juzi ingawa kwa ndege tofauti, na wameshaanza mazoezi tayari kwa mechi zinazofuata za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

"Dube na Tigere ndiyo walioanza kufika, walikuja na ndege tofauti, Kangwa yeye ndege ilichelewa alifika baadaye, lakini wote wameshaanza mazoezi kwa ajili ya mechi zinazofuata za Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Zaka Zakazi.

Wachezaji hao waliwasili nchini wakitokea kwao Zimbabwe ambako walikwenda kwa mapumziko mafupi, baada ya kutolewa kwenye michuano hiyo inayoendelea nchini Cameroon, kwenye hatua za makundi.

Wachezaji hao ni kati ya watano wa Ligi Kuu Tanzania Bara waliokwenda kucheza michuano hiyo. Wengine ni Djigui Diarra wa Yanga ambaye aliitwa na timu ya Taifa ya Mali, kwa bahati mbaya hakucheza hata mechi moja, mwingine ni Peter Banda wa Simba aliyekuwa na kikosi cha Timu ya Taifa ya Malawi.

Wakati huo huo, klabu ya Azam imemwongeza mkataba beki wao aliye kwenye kiwango cha juu kwa sasa Abdallah Kheri 'Sebbo'.

Zaka Zakazi amesema kuwa kijana huyo ataendelea kuwapo kwenye viunga na Azam Complex hadi 2024, kwani amesaini mkataba wa miaka miwili.






# Kocha Prisons atabiri mechi ngumu Simba

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Patrick Odhiambo, amesema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu dhidi ya Simba na ana matarajio utakuwa mchezo wenye ushindani mkubwa.

Tanzania Prisons imewasili Dar es Salaam jana asubuhi na iko tayari kwa ajili ya mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho, Alhamisi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wametoka kupoteza michezo miwili mfululizo na Simba nao kutopata matokeo mazuri katika mechi za hivi karibuni.

Alisema wamefanya maandalizi mazuri ikiwamo safu yao ya ushambuliaji kuhakikisha inakuwa makini kutumia vema nafasi watakazozipata.

"Tumekuwa na shida kwa washambuliaji wetu, kupoteza umakini, nafasi katika tunazozitengeneza, tumelifanyia kazi na ninaamini mechi itakuwa nzuri kiufundi na kimbinu kwa sababu wote tumetoka kujeruhiwa," alisema Odhiambo.

Alisema kuelekea mchezo huo atawakosa wachezaji wake wawili, Benjamin Asukile na Jeremia Juma ambao ni majeruhi.

# Michezo

Jumatano Februari 2, 2022

Nipashe



Mbappe, Real Madrid wakubaliana

UKURASA 22

**SAJILI ZA USIKU...**




Usiku wa kuamkia jana Rangers iliushitua ulimwengu wa soka baada ya kumsajili kiungo Aaron Ramsey akitokea Juventus huku Barcelona ikinasa saini ya mshambuliaji wa Arsenal, Pierre Emerick Aubameyang pamoja na winga wa Wolves, Adama Traore. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaanika mkakati wa ujenzi uwanja mpya

**Na Adam Fungamwango**

## Bilioni 20 zaipa jeuri, CAF nayo yaruhusu mashabiki 35,000 kuiona na Asec Mimosa kwa Mkapa...

KLABU ya Simba imesema kuwa Sh. bilioni 20 zilizowekwa na mwekezaji wake bilionea Mohamed “Mo” Dewji zinaweza kutumika kuombea mkopo wa kujenga uwanja wake itakaoutumia kucheza mechi zake za michuano yote, ikiwamo Ligi Kuu na mechi za kimataifa.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Meneja Habari wa Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kuwa mawazo na azma ya kujenga uwanja ipo pale pale, huku wanachama na mashabiki wakiendelea kuchanga, lakini wakati huo viongozi wa klabu hiyo wanakamilisha mchakato wa kuunda kamati maalum itakayosimamia ujenzi huo.**

“Mwanzo ulikuwa ni mpango wa mashabiki waliokuwa na munkari kutokana na jambo lililotokea, lakini wingi wa michango ulifanya viongozi kukaa na kuliendeleza jambo hilo, ndiyo maana kwa sasa tumeandaa michoro ya uwanja, inaundwa kamati maalum ya kulishughulikia suala hilo kwa sababu jambo hili haliwezi kuendeshwa na viongozi au bodi. Na siyo kama tunategemea michango tu ya wanachama na mashabiki hapana, wao wanaendelea kuchanga, lakini ukumbuke Simba kwa sasa ni taasisi inayokopesheka, tuna kiasi cha Sh. bilioni 20 benki ambazo tukienda kuchukulia mkopo tunajenga uwanja bila matatizo yoyote, kikubwa pumzi tu,” alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa kwa sasa kuna baadhi ya watu wanaona kama ni jambo ambalo haliwezekani, lakini kwa jinsi viongozi wa klabu hiyo walivyojipanga, wengi watashangaa.

“Tunakwenda kufanya kitu cha tofauti ambacho hakijawahi kuonekana Afrika hii,” alisema.

Kasi ya Simba kutaka kuwa na uwanja wake, ilianza baada ya Desemba 11, mwaka jana, ilipomalizika mechi ya timu hiyo dhidi ya watani zao wa jadi Yanga, huku Ofisa Mtendaji Mkuu Barbara Gonzalez akiwa amezuiwa kuingia uwanjani.

Ni kitendo kilichowaudhi na kuwakera wanachama na mashabiki wa Simba, walioanza kuhamasishana kwenye mitandao ya kijamii kuchangishana pesa kwa ajili ya kujenga uwanja. Suala hilo lilibebwa na Mshauri wa Mwekezaji, Crescentius Magori ambaye aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii kuwa wakiamua hawawezi kushindwa kuwa na uwanja wao japo wa kuingiza watu 30,000 na ndipo mwekezaji mwenyewe, Mo Dewji alipojitokeza na kukubali maoni na maombi ya wanachama na mashabiki wa klabu hiyo, akaahidi kutoa kiasi cha Sh. bilioni 2 kuchangia ujenzi huo.

Katika hatua nyingine Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limeruhusu mashabiki 35,000 kuingia Uwanja wa Benjamin Mkapa Februari 13, mwaka huu kushuhudia mechi ya Kombe la Shirikisho kati ya wenyeji Simba na Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Akizungumzia ruksa hiyo, Ofisa Habari wa Simba, Ahmed, alisema pamoja na kuruhusiwa huko, wametakiwa kufuata masharti yote ya kujikinga na virusi vya corona kwa kunawa mikono kabla ya kuingia uwanjani, kuvaa barakoa na kukaa kwa nafasi kwa kuruka nafasi moja uwanjani hapo.

Alisema kama mashabiki watatekeleza masharti hayo, wanaweza kuongezewa idadi ya mashabiki watakaoingia uwanjani kwenye mechi zinazofuata, lakini pia endapo watakiuka kuna uwezekano wakuzuiwa kabisa kushuhudia michezo ijayo.

Simba ambayo itaanzia nyumbani katika hatua hiyo ya makundi dhidi ya Asec Mimosas, baada ya mchezo huo Februari 20 itaifuata USGN ya Niger kabla ya kuhitimisha raundi ya kwanza ya michuano hiyo kwa kuifuata RS Berkane ya Morocco Februari 27, mwaka huu.

## Nabi sasa awashukia wachezaji Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anatambua msimu huu kuna ushindani mkubwa, jambo ambalo amewataka wachezaji wake kufikiria mechi zao zinazowakabili hususan Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 35 baada ya kucheza mechi 13 na haijapoteza mchezo hata mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nabi alisema hataki kuona wachezaji wake wanapoteza muda kuzungumzia matokeo ya timu nyingine kwa sababu hayawahusu na kuwataka kuzingatia zaidi mechi zinazowakabili.

Alisema Yanga ina mechi ambazo zitazidi kuwa ngumu na amewataka kuanzia sasa kuchukulia kama fainali kila mchezo ulioko mbele yao ili kuweza kupata ushindi.

“Nimewaambia kabisa nikimkuta mchezaji yeyote anafanya hivyo au mtu yeyote katika benchi langu la ufundi akiijadili Simba au timu zingine kuhusu matokeo yao, nitatoa adhabu zilizoko kwenye miongozo ya kazi.

“Hakuna mechi iliyokuwa rahisi na hakuna muda wa kujadili matokeo ya wenzetu, kila mmoja anatakiwa kufikiria hatima ya mechi zilizoko mbele yetu kuhakikisha tunashinda,” alisema Nabi.

Alisema kazi kubwa ni kuhakikisha anaimarisha safu yake ya ulinzi kuwa imara na bora zaidi kuhakikisha wanapambana na washambuliaji wa wapinzani wao kutopata bao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >